# *Waebrania, Mlango Wa Nne*

. . . ni kujua zaidi juu ya Bwana wetu mtakatifu. Na hilo ndilo kusudi le—letu la kukusanyika hapa, ni kwa kusudi hilo, na, sasa, na kwaombea watoto wa Mungu walio wagonjwa. Na asubuhi ya leo tulikuwa na baraka za—za ajabu sana toka kwenye Maandiko.

2 Tunajaribu kuchukua, kila wakati wa ibada, sehemu ya . . . Ninafundisha katika Kitabu cha Waebrania, nimekuwa nikifundisha, kwa majuma kadhaa yaliyopita sasa. Na sasa, kama Bwana akipenda, tutaendelea Jumatano usiku, halafu Jumapili asubuhi, na Jumapili usiku, kwenye—kwenye, kwa kadiri tu nitakavyokuwa hapa katika wakati huu. Si ufufuo, bali ni ufufuo, mkutano katika siku zetu za kawaida usiku. Na kwa hiyo tuna furaha sana, sana kuwa na wakati huu kukutana na marafiki zetu wazuri kutoka hapa na pale humu mijini, na karibu na Miji ya Falls hapa. Na kama—kama ikitokea kwamba tuwe na kubatilisha ama chochote kile, huenda ikawa ya kwamba yamkini Bwana akatuongoza, hivi karibuni sana, kuninii . . . pengine tungekuwa na siku chache usiku, pengine, kwenye jumba la michezo ama popote pale, baadaye kidogo, kama Bwana anaonekana kuongoza hivyo, kufikia mahali ambapo tungeweza kuwakusanya watu wetu pamoja.

Nasi tumeona watu tulipokuwa tukija, wakirudi, wakisema, "Hakukuwa na nafasi ya ku—kuingia." Kwa kweli, maskani hii ni ndogo sana. Inaketi tu watu wachache sana, sana, nasi tunafurahi sana tu ya kwamba mko tayari kuja huku na kuketi kwenye joto, kusikiliza Neno la Bwana. Nasi tunaomba ya kwamba Mungu atawabariki sana, kwa wingi na kuwasaidia.

3 Na sasa, usiku wa leo, tunataka, tunaanzia kwenye mlango wa 4 . . . Ni wangapi waliokuwa hapa asubuhi ya leo? Hebu tuone mikono yenu. Loo, hilo ni jambo zuri sana, karibu ni ninyi nyote. Nasi tuko kwenye, kuanzia kwenye, mlango wa 4 wa Kitabu cha Waebrania. Loo, ni Kitabu cha ajabu jinsi gani! Je! mnakifurahia? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Na ni kulinganisha Andiko kwa Andiko.

4 Na Paulo, kabla hajapata kushuhudia tukio lake, ilibidi kwanza ashuke kwenda Uarabuni na ajifunze, kwa Neno kama jambo hilo lilikuwa ni Kweli. Ninapenda jambo hilo. Na somo la asubuhi ya leo, tuliona, katika mafundisho asubuhi ya leo, ya kwamba Kristo alikuwa ni yeye yule jana, leo, na hata milele. Nae Paulo alikuta ya kwamba Nguzo ile ile ya Moto iliyowaongoza wana wa Israeli, ilikutana naye njiani akienda zake Dameski. Tuliona ya kwamba hiyo Nguzo ya Moto, iliyowaongoza wana wa Israeli kule nyikani, kwenda katika nchi

ya ahadi, ilikutana na Paulo njiani akienda zake Dameski, na ikajiita Yenyewe, "Yesu."

5 Ndipo tunaona Uungu mkuu kabisa na halisi wa Yesu Kristo. Kitabu chote hapa ni ufunuo tu wa Yesu Kristo. Naye alikuja, tunaona hilo, "Kwa njia nyingi na kwa sehemu nyingi, Mungu alisema na wale mababa katika manabii; katika siku hizi za mwisho katika Mwanawe, Kristo Yesu." Amejifunua Mwenyewe. Na Kitabu hiki kutoka Mwanzo hadi Ufunuo si kitu kingine chochote ila ni ufunuo mmoja wa Bwana Yesu usiobadilika na usiokoma.

6 Nasi tunaona ya kwamba Yeye Ndiye aliyekuwa katika kile kijiti kilichokuwa kinawaka moto. Tunaona ya kwamba Yeye Ndiye aliyekuwa kwa Mungu kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu. Na tunaona ya kwamba, katika Agano Jipya, Yeye alikuwa ni Mungu na Mwanadamu, kwa wakati mmoja. Ndipo basi wakati alipoliacha Agano Jipya, kwenda Zake Mbinguni, alisema, "Nimetoka kwa Mungu, na ninarudi kwa Mungu."

7 Halafu basi wakati Paulo alipokutana Naye, Yeye alikuwa katika umbo lile lile ambalo alikuwa nalo wakati alipokuwa akiwaongoza Israeli, Nguzo ya Moto. Ndipo Paulo akamwangalia moja kwa moja usoni, akiwa hajaongoka, na Hiyo ilimsababisha apate matatizo ya macho siku zake zote zilizosalia. Alipofuka, na kwa siku nyingi hakuweza kuona chochote kabisa. Ilibidi aongozwe kupelekwa kwenye barabara iitwayo Nyofu.

8 Basi Mungu alikuwa na nabii kule aliyenena naye, kwa jina la Anania, aliyekuja na kuingia, kwa ono, na akaweka mikono yake juu ya Paulo, na kusema, "Ndugu Sauli, pokea kuona kwako."

9 Na tunaona ya kwamba, basi, ya kwamba Roho Mtakatifu yeye yule, Bwana Yesu yeye yule, alimjia Petro katika umbo la Nuru na kumtoa gerezani.

10 Pia tunaona ya kwamba Bwana Yesu yeye yule, katika siku hizi, angali yuko katika ile Nguzo ya Moto (Nuru) inayowaongoza watu Wake (Kanisa Lake), ikifanya jambo lile lile, ikitoa maono; ikija na kuweka mikono juu ya watu, kwa ono. Bwana Yesu, Ambaye alikutana nami Jumapili iliyopita nyumbani, na kusema, "Kulikuwa kuna mtu aliyekuwa akija, mwenye nywele nyeusi, anaanza kuota mvi. Alikuwa ni Myunani. Mkewe alikuwa wa umri wa makamo, naye atakuwa akilia madhabahuni."

11 Baadhi yao walikuwa wamekwisha kulinena, nao walijua lilikuwa likitukia. Alikuwa ni kiwete, ne—neva ya fahamu kichwani mwake ilikufa. Hata asingeweza kutumia miguu yake wala mikono yake. Na alikuwa ni kipofu. Na ili kulithibitisha jambo hilo maradufu: nilimwita maskini mama mmoja aje awaombee wagonjwa, kwanza, kisha nikageuka

nyuma na kumtaka Ndugu Toms aje aombe. Nasi, tukiketi hapa, tukiliangalia litukie. Na kisha nikashuka kwenda kuwaombea wagonjwa, kisha nikarudi. Ndipo mkewe akaja, kulingana kabisa na lile ono, na kunikamata mkono na kuanza kulia, na kusema Dk. Ackerman alikuwa amewatuma waje hapa. Dk. Ackerman ni rafiki wangu msiri, Mkatoliki. Mvulana wake ni kasisi kwenye nyumba ya watawa huko—huko Mtakatifu Meinrad, na anakaa huko chini Indiana. Na mtu huyu alikuwa ametoka Jasper. Na Bwana akamponya, kutoka kwenye kiti hicho. Aliinuka na kutembea. Aliweza kuona vizuri kama mtu mwingine yeyote. Kisha akatembea kutoka humo jengoni, mzima na mwenye afya. Yote kwa ono!

12 “Ndugu Sauli, Bwana Yesu aliyekutokea njiani, amenituma nipate kuweka mikono yangu juu yako, upate kuona kwako na ujazwe na Roho Mtakatifu.” Ajabu sana.

13 “Ndipo tunaona, kwa kuwa tuna wokovu mkuu namna hii, haitupasi. . . Tusingeweza kupona hasira na adhabu za Mungu, tusipoujali wokovu mkuu namna hii.”

14 Sasa tutaanza kusoma, usiku wa leo, kwenye, na tuanzie mlango wa 4 wa Kitabu cha Waebrania. Kama mtu yeyote anataka kufuatilia, tuna Biblia chache hapa. Kama mtu angetaka moja, mbona, mmoja wa mabawabu ataileta kwako, ukiinua mkono wako, Biblia hizi—hizi hapa. Kama mmoja wa ndugu hapa atachukua. . . Kuna Biblia mbili zilizopo hapa, ninaamini.

15 Na sasa tutaharakisha, kwa maana tuna ushirika baada ya muda mfupi. Na tutakapomalizia usiku wa leo, tutaanzia hapo tena Jumatano usiku. Sasa, ninaamini, asubuhi ya leo katika kusoma kwetu, tulianzia kwenye kifungu cha 15.

16 Mtu fulani, labda hajanijua nikivaa miwani, ya kusomea. Ninazeeka. Nami ningali ninaweza kusoma, bali siwezi kusoma haraka, hasa wakati nina maandishi madogo hapa, herufi ndogo.

17 Nami nilienda kufanyiwa uchunguzi wa macho, kuona kama kweli macho yangu yalikuwa yanaanza kupofuka. Macho yangu yalikuwa kumi-kumi. Alisema, “Lakini umepita umri wa miaka arobaini, mwanangu.” Aliniwekea kitu alichotaka nisome, akasema, “Anza kusoma hayo.” Nikasoma. Nami nikaendelea kukaribia, nikazidi kusoma pole pole zaidi na zaidi. Ndipo ikafikia umbali kama *huu*, nikakoma. Ndipo akaleta pale cha kumi-kumi, ningeweza kuyasoma mahali popote. Lakini akasema, “Jambo ni kwamba, unapopita umri wa miaka arobaini, mboni zako za macho zinakuwa bapa.”

18 Sasa, ninaweza kuyasinyaza macho yangu na kusoma karibu nami namna *hii*, bali inakupasa kusinyaza macho. Kwa hiyo, alinitengenezea tu miwani moja. Ninaweza kuona nayo, mahali popote, wakati yako karibu sana na mimi. Sasa, yanapokuwa

mbali nami, siwezi kuona hata kidogo kwa vitu hivi. Lakini ninayasoma, nikisoma katika hiki kwa miwani.

19 Sasa, asubuhi ya leo, tulikuwa na sehemu ya mwisho ya mlango wa 3 wa Waebrania. Na, loo, ni viini tajiri jinsi gani tupatavyo. Sasa sikilizeni. Ninataka kusoma tena, kusudi tupate msingi sasa. Si kuzungumza habari zake, lakini ni kulipitia kidogo kwa namna fulani tu.

> *Hapo inenwapo, Leo, kama ninyi . . . taisikia sauti yake, msifanye migumu mioyo yenu, kama wakati wa kukasirisha.*
>
> *Maana ni akina nani,* hao*, walisikia* Neno*, waliokasirisha, waliposikia* Neno? *Si wale wote waliotoka Misri wakiongozwa na Musa?*

20 Sasa, katika jambo hilo, asubuhi ya leo, tunaona ya kwamba Yeye alisema, "Msifanye migumu mioyo yenu sasa, kama wakati wa kukasirisha." Hapo ndipo walipomkasirisha Mungu, kwa maana alikuwa amewapa Musa, nabii Wake, na ishara iliyokuwa pamoja na Musa. Ni wangapi, walio darasani humu usiku wa leo, wanaojua ishara hiyo ilikuwa ni nini? Nguzo ya Moto, Waebrania 13

21 Sasa, hatujui kama kusanyiko hilo liliiona ishara hiyo ama hawakuiona. Lakini Musa aliiona, kwa maana Musa alikutana Naye mara ya kwanza katika kijiti kilichowaka moto. Yeye alikuwa ni Moto. Nao wana wa Israeli walimtii Musa, na kuondoka Misri. Na mara walipotoka Misri, Mungu, tuliona, aliwaongoza akawaingiza moja kwa moja kwenye mtego. Ambapo, jeshi la Farao likiwa nyuma yao, Bahari ya Shamu pande zote mbili, na Mungu akawaweka katika jaribio; nao wakaogopa. Na hilo lilimkasirisha Mungu. Akasema, "Mbona unanililia Mimi?" Kasema, "Nena tu na msonge mbele." Ninapenda hilo.

22 Sasa, walikuwa wakimfuata Musa, kama Musa alivyofuata Nguzo ya Moto na Wingu, nao walikuwa wakienda zao kwenye nchi ya ahadi. Picha nzuri ya Kanisa, usiku wa leo, tukienda zetu kwenye Nchi ya ahadi, tukiongozwa na Roho yeye yule, ishara zile zile na maajabu kama Mungu alizonena habari zake.

23 Sasa angalia. Ndipo, wakafika kwenye Bara ya Sini. Ma—maji yalikuwa "machungu," *Mara*. Kwa nini Mungu aliwaongoza kwenye maji machungu? Inaonekana kana kwamba angaliwaongoza kwenye maji mazuri. Bali aliwaongoza kwenye maji machungu kusudi apate kuijaribu imani yao. Yeye hupenda kufanya jambo hilo. Hupenda kuacha dhiki zije juu yako, apate kuonyesha anaweza kukuonyesha upendo Wake na nguvu Zake. Watu wanawezaje, siku hizi, ambao hawaamini katika Mungu anayefanya miujiza . . . Dhiki zinapokuja, wanakata tamaa tu na kufanya kama zamani. Bali sisi tunaamini ya kwamba "Mungu hufanya miujiza." Yeye hawezi . . . Mungu ameninii . . .

24 Sikilizeni jambo hili. Kama Mungu hatendi namna ile ile, wakati hali zile za mambo zinapozuka, basi Mungu ana hatia ya kuwa na upendeleo kwa watu Wake. Ukuu wa Mungu unamhitaji Yeye kutenda kazi katika kila jambo kama alivyofanya kwenye jambo la kwanza, la sivyo alikosea wakati alipotenda katika jambo la kwanza. Mungu asipotenda namna ile ile katika tukio la kwanza, kama anatenda vinginevyo katika tukio la pili, basi alikosea alipotenda katika jambo la kwanza. Kama Mungu aliwaponya wagonjwa katika Agano la Kale, inambidi kufanya jambo hilo katika Agano Jipya leo, la sivyo alikosea wakati alipowaponya huko nyuma. Hana budi kutenda vile vile, kila wakati. Naye atafanya jambo hilo, wakati imani ile ile itakapotimiza sharti hilo. Kosa liko kwetu, haliko kwa Mungu. Kwa kuwa tunamwona kwa wengine, na wengi, akifanya miujiza mikubwa isiyo ya kawaida. Tunajua jambo hilo. Mkosoaji asingeweza kusema, "Sivyo." Kwa kuwa tunaliona likithibitishwa, na ndilo hilo hapo.

25 Walikuwa wakisema, "Nionyeshe muujiza." Hawawezi kusema hivyo tena. Sayansi haiwezi kusema hivyo tena. Tunaweza kuuthibitishia kabisa ulimwengu wa sayansi. Nao ulimwengu wa sayansi umeshuhudia ya kwamba Kiumbe cha kimbinguni, katika umbo la Nguzo ya Moto, kiko pamoja nasi. Hii hapa picha Yake, papa hapa, na moja inaning'inia huko Washington D.C., usiku wa leo. Ni Kristo yeye yule.

26 Kwa hiyo, kama vile muda mfupi, ndugu zangu wahudumu walivyokuwa wakiniambia, "Loo, Ndugu Branham, huyo ni Ibilisi. Usijipumbaze na jambo hilo." Waliniogopesha.

27 Nami nisingeweza kuhubiri jambo hilo mpaka Mungu alipokuja na kulifunua, ya kwamba, "Ni Yesu yeye yule, Yeye yule." Loo, sasa hebu ujaribu kulitikisa ulitoe ndani yangu? Haiwezekani. Kwa kuwa, ni Maandiko. Ni Neno la Mungu. Si ujuzi tu uliofyatuka akili. Ni ujuzi unaoungwa mkono na Neno la Mungu na ahadi ya Milele iliyobarikiwa ya Mungu.

28 Sasa, tunaona hapa, basi, ya kwamba Yeye alisema.

*Kwa kuwa wengine, waliposikia, walimkasirisha:. . .*

Bila shaka. Walichoka, kila wakati walipofikia mahali ambapo shindano la kuamua lilikuja. Ndipo wangefanya nini? Wangefarakana, na kuchoka, na kutaka kurudi nyuma, na "Kwa nini jambo *hili* lilinipata?"

29 Jambo la kushangaza, asubuhi ya leo, baada ya kuhubiri hilo kwa nguvu tu jinsi nilivyoweza, kulikuwa na wengi waliokuja madhabahuni na kuhoji Hilo, "Ni kwa nini jambo hili linanipata?" Unaona jinsi linavyokuwa? Linawapita watu. Ni namna ile ile tu, watu.

30 Yesu alisema, "Mna macho, lakini hamwezi kuona." Aliwaambia wale wanafunzi hilo.

31 Wakasema, "Tazama, sasa unasema waziwazi. Sasa tunaamini. Hakuna mtu anayepaswa kukwambia jambo lolote, maana Mungu anakuonyesha Wewe hilo."

32 Akasema, "Je, sasa mnaamini, baada ya muda huu wote?" Unaona?

33 Hampaswi kumhoji kitu chochote, Mungu. "Kwa kuwa hatua za mwenye haki zinaongozwa na Bwana." Na kila jaribio linawekwa juu yako, kukuthibitisha. Na Biblia ilisema, "Yana thamani zaidi kwako kuliko dhahabu." Kwa hiyo kama Mungu aliruhusu mateso machache mepesi yakupate, kumbuka, ni kwa ajili ya kukurudi wewe. "Kila mwana amjiaye Mungu hana budi kurudiwa na Mungu kwanza, na kujaribiwa, apate mafunzo ya mtoto." Hakuna asiyerudiwa. "Kila mwana ajaye." Mateso haya yanafanywa ama kusababishwa—kusababishwa, kuona utachukua msimamo gani. Unaona? Ni Mungu, kwenye mahali hapa pa kujaribia. Hiyo ni dunia nzima, ni mahali pa kujaribiwa, na mahali Yeye anapojaribu kukujaribu.

34 Sasa sikilizeni, tunaposonga mbele. Nami ninataka kupata sehemu yake ya mwisho.

> *Tena ni akina nani aliowaapia ya kwamba hawataingia katika raha yake, . . .*

Sasa, hapo ndipo tunapopaendea, usiku wa leo.

> *. . .katika raha yake, ila wale walioasi?*
>
> *Basi twaona ya kuwa hawakuweza kuingia . . .sababu ya kutokuamini kwao.*

35 Sasa, dhambi ni nini? Kutokuamini. Mungu alikuja kwao, katika Nguzo ya Moto; akamtuma nabii Wake, na kumtia mafuta, akampa ishara za kufanya mbele ya watu. Na ndipo Nguzo ya Moto, kwa nabii huyo, ikawaongoza kuwatoa. Kila mazingira waliyoyaingia, walianza kunung'unika na kukosoa kila kosa dogo walilopata kwa Musa, wakaanza kumkemea na kumropokea. Ndipo Mungu akachukizwa, kwa sababu Yeye alisema, "Walikuwa wakitenda dhambi."

36 Walipaswa kumsikiliza. Lakini, badala ya kufanya hivyo, walisikiliza hoja, "Inawezekanaje? Mambo haya yanawezaje kuwa hivi?" Kama Yeye ni Mungu, kila kitu kinawezekana. Naye atafanya kila kitu kitende kazi kwa pamoja kwa manufaa ya wale wampendao.

37 Sasa tunaingilia somo kubwa sana hapa, hilo ni, juu ya "Raha," ile *sabato*. Sasa, wao walikuwa ni wasafiri katika safari yao. Unaona? Walikuwa kule Misri, miaka mia nne, nao walikuwa katika utumwa. Na sasa walikuwa wakitolewa kwa miujiza ya Mungu, kulingana na ahadi Yake. Nao walikuwa wakienda zao kwenye nchi ya ahadi. Ndipo hii hapa Nuru ya mbinguni inatokea, miongoni mwao, na kuanza kuwaongoza.

38 Sasa, mtu fulani angesema, “Sasa, angalia hapa, huyu Musa ni nani? Ni nani aliyekufanya mtawala juu yetu? Je! wewe si ni mmoja wetu? Ni nani aliyekuweka wewe hapa uwe bosi wetu? Unafikiri wewe unajua zaidi ya mchungaji wetu? Unafikiri wewe unajua zaidi ya kuhani wetu? Unafikiri wewe ni—wewe una akili kuliko watu wetu wa dini, wa siku hizi?” Hilo halikuwa na uhusiano wowote nalo.

Ilikuwa ni Mungu, katika Nguzo ya Moto, akithibitisha ya kwamba Yeye alikuwa Ndiye aliyekuwa kazini. Haikuleta tofauti yoyote ni nani aliyekuwa na akili na ni nani asiyekuwa na akili. Ilikuwa ni shauri la kufuata kile Mungu alichoweka mbele zao.

39 Mbona, Musa, tukinena kimwili, alifanya jambo la kipumbavu alipojaribu kuwakomboa hao wana kwa Neno la Mungu, akitoa kundi la watu na kulipeleka jangwani. Wakati alipokuwa na ninii yake . . . Mbona, yeye alikuwa ndiye mrithi wa kila kitu walichokuwa nacho. Alikuwa ameshinda kabisa kila jeshi lililokuwako, ulimwenguni kote. Na huyo hapo, jemadari mkuu wa kijeshi. Ndipo hatua nyingine, alikuwa awe mfalme, Farao wa Misri. Mbona, angaliweza tu kuketi kwenye kiti cha enzi, na angesema, “Vema, enyi wana rudini nyumbani kwenu.” Hilo linamaliza yote; yeye alikuwa ni Farao. Lakini Musa . . .

40 Loo, jambo ndilo hili hapa. Musa, kwa *imani*, aliona ahadi ya Mungu. Ndipo Malaika wa Bwana akamjia, naye akajua mengi zaidi kuhusu Mungu, katika dakika tano Uweponi mwa Malaika huyo, kuliko aliyojifunza katika miaka arobaini na waalimu wa Misri. Yeye alijua ya kwamba Yeye alikuwa ni Mungu. Aliona miujiza ikifanyika.

41 Akasema, “Nitakuwa pamoja nawe, Musa. Nitaenda mbele zako.” Nao wakafahamu. Naye akampa ishara za kufanya.

42 Sasa, walikuwa wakienda zao kwenye nchi ya raha. Mungu aliwapa raha, mahali ambapo isingewapasa kuwa ninii . . . wasimamizi juu yao, kuwaswaga, kuwafanya wafanye mambo wasiyopenda.

43 Ni picha nzuri jinsi gani siku hizi, tunapoliangalia Kanisa na kuliona Kanisa katika hali yake, kila mtu aliyezaliwa kwa Roho wa Mungu huudharau ulimwengu. “Na ukiupenda ulimwengu ama mambo yaliyo katika ulimwengu, kumpenda Mungu hata hakumo ndani yako.” Hivyo ndivyo Biblia ilivyosema. Na msafiri wa kweli, akiwa safarini, kwa kawaida huyachukia mambo ya ulimwengu. Anachukia kuwaona wanaume wakinywa pombe. Anachukia kuwaona wanaume wakivuta sigara. Anachukia kuwaona wanawake mtaani, wamevaa hizo nguo fupi na chafu. Anachukia kuona karata na karamu za kadi.

44 Na jana, wakati Ndugu Tony . . . ama mimi na Ndugu Woods tulipokuwa tukipita mtaani, na wengine zaidi, baadhi ya wanaume fulani . . . Kulikuwako na maskini bibi mmoja huko

Louisville, akitembea barabarani, wasichana wazuri sana, wakiwa wamevaa nguo zilizokuwa chafu sana; juu kidogo tu ya nyonga, na utepe mdogo umefungwa kwenye nyonga zake, kila upande, na kipande kidogo cha mviringo cha nguo mbele zake, na kimefungwa na kamba nyuma. Akitembea mtaani, katika namna chafu sana, na kila mwanamume barabarani akimwangalia. Nikasema, "Yeye hatambui ya kwamba ana hatia, machoni pa Mungu, ya kufanya uzinzi na kila mwanamume aliyemwangalia akiwa jinsi hiyo. Naye atajibu katika siku ya hukumu kwa kufanya uzinzi na wanaume hao."

45 Yesu alisema, "Kila amwangaliaye mwanamke kwa kumtamani, amekwisha kuzini naye." Hiyo ni kweli.

46 Kwa hiyo, unaona, Ndugu Woods akaniambia, "Unasemaje juu ya jambo hilo, Ndugu Branham?"

47 Nikasema, "Ama ni kupungukiwa na akili au kupagawa na pepo." Kuna vitu viwili tu vya kusababisha jambo hilo. Mwanamke mwadilifu, msafi hatavaa vitu hivyo; isipokuwa awe amepagawa na pepo. Hiyo ni Kweli kabisa.

48 Sasa, msafiri anayesafiri kwenda zake Mbinguni, yeye anaishi katika mazingira mengine. Haikulazimu kuwa na wasiwasi juu ya yeye kumwangalia mwanamke huyo. Yeye atageuza kichwa chake kama ana Mungu moyoni mwake, kwa kuwa anaishi katika mazingira ambayo ni maili milioni moja kutoka kwenye mambo hayo. Hiyo ni kweli. Hutaki kuwa na hatia ya upuuzi huo, hukumuni. Kwa hiyo yeye hugeuza kichwa chake na kusema, "Mungu, mrehemu mwanamke huyo," kisha anasonga mbele. Tuko safarini. Tuko njiani tukielekea Nchi ya Kanaani. Tuko njiani kwenda kwenye ile Raha iliyobarikiwa ya Milele ambayo Mungu ametupa. Na katika safari hiyo, tunajaribiwa. Tunajaribiwa kwa mambo ya kila namna, bali hata hivyo tunajaribiwa, bila kufanya dhambi.

49 Sasa angalia, tunapoelekea kwenye mlango wa 4, "Na tuogope."

> *Basi, ikiwa ikaliko ahadi ya kuingia katika raha yake, na tuogope, . . .*

50 Ninawatakeni mkumbuke, ya kwamba, tusipotafuta kujua, Mungu asipotufunulia! Haidhuru tunaenda kanisani mara nyingi jinsi gani, hilo halihusiani. Mungu hana budi kuja kwa ufunuo na kujifunua Mwenyewe kwetu, hilo linatoa nje mambo yote ya ulimwengu. "Sasa, wakati inenwapo, 'Leo kama . . .'"

51 Sasa hebu na tuanzie m—mlango wa nne.

> *Basi, ikiwa ikaliko ahadi ya kuingia katika raha yake, na tuogope, . . .*

52 Sasa kumbukeni, walipokuwa wakienda zao kwenye Raha, Nguzo ya Moto iliwaongoza. Sasa tunataka kuona, "Raha hii ni nini?"

> *Basi, ikiwa ikaliko ahadi ya* kuingia *katika raha yake,. . .tuogope, angalieni mmoja wenu asije akaonekana ameikosa.*

53 Sasa, hii hapa ahadi. Hapa ndipo inapotupasa kuogopa: kama hakuna ahadi tuliyoachiwa. Bali kuna ahadi! Na halafu, jambo lingine, msipungukiwe nalo.

54 Sasa, wazo ni kwamba, kama tuko njiani tukielekea kwenye Raha, Raha ni kitu gani? Iko wapi? Je! ni kujiunga na kanisa? Je! ni kubatizwa kwa njia fulani? Je! ni kuwa mfuasi wa kanisa lililo kubwa sana jijini? Kuvaa nguo nzuri zaidi? Je! ni elimu? Je! ni pesa, ili kwamba tuweze kuacha kazi na kulala tu, tustarehe maishani mwetu mwote, tunavyoiita? Siyo hiyo.

55 Sikilizeni Biblia inavyosema ni nini, na jinsi tunavyoipata.

> *Basi, ikiwa ikaliko ahadi ya kuingia katika raha yake, na tuogope, mmoja wenu asije akaonekana ameikosa.*
>
> *Maana ni kweli, sisi nasi* (wa zama hizo) *tumehubiriwa habari njema vile vile kama hao . . .*

Injili ni nini? Habari njema. Habari njema iliwajia huko Misri, ya kwamba, "Mungu amemtuma mkombozi, Naye atatutoa na kutupeleka kwenye nchi ya ahadi."

56 Habari njema kwetu sasa, ya kwamba, "Mungu amemtuma Mkombozi, Roho Mtakatifu, nasi tuko njiani tukielekea kwenye Nchi ya ahadi." Sasa watu wamelifanya kanuni za imani na madhehebu, bali Mungu angalia anashikilia, ya kwamba, *Raha* yetu ni "Roho Mtakatifu."

57 Angalia.

> *. . .tumehubiriwa habari njema vile vile kama hao. Lakini neno lile lililosikiwa halikuwafaa hao,* ninii . . .

Kumbukeni:

> *. . .neno lile lililosikiwa halikuwafaa hao, kwa sababu halikuchanganyika na imani ndani yao waliosikia.*

58 Loo, ndugu zangu, hebu nisimame hapa kwa dakika moja. Haidhuru Neno lihubiriwe jinsi gani, jinsi gani ambavyo unapenda jinsi lilivyohuburiwa; wewe mwenyewe usipokuwa mshiriki wa Hilo, halitakufaa kitu hata kidogo.

> *. . .halikuchanganyika na imani ndani yao waliosikia.*

59 Waliona miujiza ya Musa. Wakasema, "Hiyo ni mizuri sana." Nao wakaenda tu. Wao, walimwona akifanya miujiza. Kisha wakaiona ile Nguzo ya Moto, labda, ama wakawasikia wakinena habari Zake. "Loo, hilo ni sawa."

60 Lakini halikuchanganyika na imani ya mtu binafsi. Kwa kuwa mara walipofika jangwani, wao (kila mmoja) walianza kunung'unika. Ndipo Mungu akasema, "Kwa kuwa walitilia shaka, ilikuwa ni dhambi." Usitilie shaka jambo lolote. Amini. Usitilie shaka, haidhuru kisa hicho ni kigumu namna gani, liamini tu.

61 Sasa walianza kunung'unika, na Mungu akawatupilia mbali. Ndipo akaapa, katika hasira Yake, ya kwamba, "Hawataingia kamwe katika Raha Yake." Na Biblia ilisema hapa, ninaamini ni katika m—mlango wa tatu, ya kwamba, "Mizoga yao ilianguka katika jangwa."

62 Mlango wa 3 na kifungu cha 17.

> *Tena ni akina nani aliochukizwa nao miaka arobaini? Si wale waliokosa, ambao mizoga yao ilianguka katika jangwa?*

63 Na katika wale wote waliotoka Misri, ni wawili tu walioingia katika nchi ya ahadi. Kutoka katika ulimwengu wote uliotangulia ile gharika, katika siku zilizopita, kulikuwako na watu wanane waliookoka, kutoka katika mabilioni. "Mlango ni mwembamba na njia imesonga, na ni wachache watakaoiona."

64 Watu wengine husema, "Basi, Ndugu Branham, ni vipi kuhusu haya maelfu yote ambao Biblia ilisema wataonekana kule?"

Hebu kumbuka tu ni wangapi wamekufa katika kila kizazi, ambao walikuwa ni Wakristo, katika wakati wote huko nyuma. Wote watafufuka. Hao ndio wanaoufanya ule Mwili. Unatarajia kutakuwa na bilioni mia moja katika Marekani hii, watakaotoka, ama baadhi ya wengine, ulimwengu huu siku hizi. Huenda kusiwe na hamsini watakaotoka. Lakini Kanisa kuu lililokombolewa limelala mavumbini, likingojea. Wao ni vito vya Mungu ambavyo vimepumzika mavumbini. Bali nafsi zao ziko chini ya madhabahu ya Mungu. Hawako katika hali yao halisi. Wamo katika mwili, kweli, bali ni thiofani. Nao wanamlilia Mungu, "Hata lini?" Wangeweza kuonana wao kwa wao, bali wasingeweza kupeana mikono, mwili wa aina hiyo.

65 Ukikutana na mama yako Utukufuni usiku wa leo, kama ukiondoka, usingeweza kumpa mkono maana hana mkono wa aina hiyo. Usingeweza kuuhisi kama ambavyo ungaliuhisi sasa. Kwa sababu, hisi tano ndizo ambazo zimewekwa katika mwili huu, ambazo zingeweza kuuongoza. Uwepo wake ungesikika katika mazingira tofauti.

66 Ni kama mume na mke. Hakutakuwa na kuoa, ama kuolewa, Mbinguni. Kwa nini? Kwa maana kuna upendo wa aina nyingine. Hakuna tamaa ya kujuana kimwili. Mambo hayo yote yamepita. Umesafishwa na u msafi.

Bali kamwe hujapata kuishi katika hali hiyo, kwa hiyo hukuumbwa kuwa hali hiyo. Unangojea tu kule. Lakini unatamani kurudi mahali ulipoumbwa mwanamume na mwanamke, na hapo Mungu ataufufua mwili huo kutoka katika mavumbi ya ardhi na kuutukuza. Ndipo utaona, utaonja, utagusa, utanusa na kusikia, na kushirikiana. Hatutajua kamwe . . .

Tusingeweza kamwe kufurahia maisha ya Malaika. Hatukuumbwa Malaika. Mungu aliwaumba Malaika. Lakini Yeye alikuumba wewe na mimi, wanaume na wanawake. Hiyo ndiyo hali tutakayokuwa nayo, milele, kwenye kule Kuja Kwake kulikotukuzwa.

67 Sasa, unaona jinsi walivyopungukiwa, kwa sababu walifanya dhambi na kupungukiwa na utukufu. Mungu aliwaonyesha Nguzo ya Moto. Aliwaonyesha ishara na maajabu. Aliwatoa. Akawaingiza katika jaribio, kuwajaribu na kuwathibitisha.

68 Sasa, hivi hujapata majaribio mengi sana? Usiyanung'unikie. Shangilia. Mungu yuko pamoja nawe. Anajaribu kuithibitisha imani yako. Mwangalie Ayubu katika Agano la Kale, wakati Yeye aliposema, "Je, umemwangalia huyo mtumishi wangu Ayubu, mtu mwenye haki, mtu mkamilifu? Hapana mmoja aliye kama yeye duniani."

69 "Loo," akasema, "hakika, umemzingira: hana shida yoyote, hana wasiwasi wowote. Hana shida zozote za kifedha, kila kitu ni shwari. Hana magonjwa yoyote, uchungu wowote. Niruhusu nimshughulikie. Nitamfanya akulaani, bila kuogopa."

70 Akasema, "Yuko mkononi mwako, bali usiutwae uhai wake.'"

71 Loo! Yeye alifanya kila kitu ila kuutwaa uhai wake, bali hakuweza kumtikisa Ayubu. Ayubu alijua alisimama imara katika Neno. Hiyo ni kweli. Na pepo wote kutoka kuzimu hawakuweza kumtikisa, kwa kuwa alijua alikuwa ametoa ile sadaka. Alikuwa mwenye haki. Basi wakamshtaki, wakasema, "Umetenda dhambi, Ayubu, na Mungu anakuadhibu." Yeye alijua ya kwamba Mungu hakuwa ameninii . . . ya kwamba hakuwa ametenda dhambi mbele za Mungu. Alijua ya kwamba alikuwa ni mwenye haki. Si kwa sababu eti alikuwa ni mtu mzuri, bali ni kwa sababu alikuwa akiikubali sadaka ya kuteketezwa kwa niaba yake.

72 Na, usiku wa leo, tunajua ya kwamba maisha yake yalithibitisha ya kwamba alikuwa mwenye haki. Na wakati wewe . . . Si kujaribu kwenda nyumbani Utukufuni ati kwa sababu unajaribu kumsaidia jirani yako; hilo ni jema. Si kwa sababu unajiunga na kanisa; hilo ni jema. Bali unaingia nyumbani Utukufuni kwa sababu unakubali haki ya Yesu Kristo, hakuna jambo lolote ulilofanya wewe mwenyewe.

73 Sasa, tunapoendelea kusoma.

> *Maana ni kweli, sisi nasi tumehubiriwa habari njema*. . .(kifungu cha 2). . .*vile vile kama hao. Lakini neno lile lililosikiwa halikuwafaa hao, kwa sababu halikuchanganyikana na imani ndani yao waliosikia.*

Imani haikuwa ndani ya hao waliolisikia Neno.

74 Hebu wazia tu, siku hizi, katika huduma hii ndogo, nyenyekevu ambayo Bwana amenipa, kunapaswa kuwepo na Wamarekani millioni arobaini waliookoka, usiku wa leo. Unajua wanasema nini? "Mbona, ni telepathia ya akili. Yeye ni msomaji wa akili. Hakuna upuuzi kama huo! Mbona, yeye si mfuasi wa kanisa letu." Unaona? Si ninii. . .haidhuru utaliwekaje kwenye Neno na kuthibitisha kwamba ni Neno la Mungu, ni ahadi ya Mungu, kwamba sayansi itathibitisha jinsi gani kwamba ni kweli, bado hawawezi kuamini. Biblia ilisema hawangeamini.

75 Unasema, "Basi kuna haja gani ya kulihubiri?" Mungu hana budi kuwa na shahidi, apate kuwahukumu, kwenye Siku hiyo. Neno lilihubiriwa na kuthibitishwa miongoni mwao, nao wangali waliliacha wakaenda zao kijinga. Hakuna kitu kilichosalia ila hukumu. Mungu asingeweza—asingeweza kulihukumu taifa lolote kwa haki isipokuwa iwe lilipewa rehema kabla ya hukumu. Yeye ni Mungu. Asingeweza kufanya hivyo.

76 Sasa tunasema nini?

> *Maana sisi tulioamini* tumeingia *katika raha ile, kama vile alivyosema, kama nilivyoapa kwa hasira yangu, hawataingia rahani mwangu: ijapokuwa zile kazi zilimalizika tangu kuwekwa misingi ya ulimwengu.*
>
> *Kwa maana ameinena* juu—juu *ya siku ya saba mahali fulani hivi,* . . .

77 Sasa, sitaki kuudhi hisia za watu, dhidi ya dini yao. Hilo silo kusudi langu. Huko nje kwenye huduma, ninahubiri tu mafundisho makuu ya kawaida, ya kiinjilisti na ya kimsingi. Lakini katika maskani hii, miongoni mwa watoto wangu hapa, ninajisikia nina haki ya kuhubiri kile ninachofikiri ni Fundisho na Kweli. Unaona? Ninayofikiri kwamba ni sawa.

78 Sasa, nina maelfu ya marafiki wazuri Wasabato, ya watu ambao ni Wasabato. Baadhi ya marafiki wapendwa sana nilio nao, baadhi yao ni Wasabato.

Ingawa, lile vuguvugu kubwa la kile tunachoita, *Sa—Sauti ya Unabii*, wananipinga kwa dhati. Walisema ya kwamba ninatoa tamshi mimbarani, na kusema, "Mimi nilikuwa Mungu. Na kwamba ninii. . .na kwamba Nuru hii iliyofuata ilikuwa ni Malaika, nami nilikuwa ni Mungu. Na ati nilikuja ulimwenguni kufanya mambo makubwa, kuwathibitishia watu kwamba nilikuwa Mungu." Sasa, hivyo ndivyo *Sauti ya Unabii*

lilivyosema kunihusu, huko California. Na yeyote aliyesema jambo hilo, ninyi mnajua, hakusema kweli.

79 Lakini kwanza, si kuwazia dhidi ya kanisa la Wasabato wala kanisa lingine lolote la Wasabato, bali ni kwa ajili tu ya Injili. Tutaingia, katika dakika chache, kwa Wapentekoste, pia. Naam. Hakika. Kuhusu Baptisti, tutangia kindani kuhusu hilo na kuonyesha ya kwamba Mungu hapendelei madhehebu yoyote. Hiyo ni kweli. Yeye anampendelea mtu binafsi tu. Wala hashughuliki na madhehebu yoyote, kamwe hajalishughulikia wala kamwe hatalishughulikia, kulingana na Neno Lake. Bali anashughulika na watu binafsi katika kila madhehebu. Naam, Mungu hushughulika na watu binafsi.

80 Sasa sikilizeni jambo hili kwa makini sana, na kama kwa hali yoyote, wakati wo wote, swali hilo likipata kuja kwako, litatatuliwa. Sasa, Bwana na atusaidie.

81 Sasa, kwa makini, "Kwa maana . . . " Kifungu cha 4.

> *Kwa maana ameinena siku ya saba mahali fulani hivi, . . .*

82 Sasa angalia. Yeye ananena juu ya sabato. Ni wangapi wanaojua ya kwamba neno *s-a-b-a-t-o* katika Kie-. . .ni neno la Kiebrania linalomaanisha "r-a-h-a"? Ni wangapi wanaojua jambo hilo, katika Kiingereza? Hakika. Hivi *sabato* halisikiki kuwa ni neno geni? Ndiyo ni geni.

83 Hivi *kutakasa* halisikiki kuwa ni neno la kigeni? *Kutakasa* ni neno la Kiyunani. *Kutakasa* linamaanisha "kufanywa mtakatifu." Kiebrania, linamaanisha "kufanywa mtakatifu." Kiyunani, linamaanisha "kutakasa." Kiingereza, linamaanisha "kufanya safi."

84 *Sabato* maana yake ni "siku ya raha." Hivyo ndivyo ile sabato ya kale ilivyokuwa, siku ya raha. Wakati unapoona *raha*, linamaanisha "sabato." Liangalie kwenye gombo lako la asili, kama ukipata kuwa na Biblia ya Kiyunani, na uone kama neno . . . Kama una Biblia ya Scofield, angalia kwenye maandishi ya pambizoni juu ya "raha" na uone kama halikurudishi kwenye *sabato*. *Sabato* maana yake ni "raha." Vema.

85 Sasa angalia.

> *Basi, ikiwa ikaliko ahadi* kwetu *ya kuingia katika* sabato *yake, raha, na tuogope, . . .*

86 Sasa, watu wengi wanaadhimisha siku, kama vile kuweka *Jumamosi* kuwa siku ya sabato. Wengine wanaifanya *Jumapili* kuwa kinyago, siku ya kuabudu. Na kwa neema ya Mungu, na kwa Neno la Mungu, Mungu anisaidie usiku wa leo, ninaweza kuwathibitishia ya kwamba wote wawili wamekosea. Wote wawili waabudu Jumapili na waadhimishaji wa sabato. Wote wawili wamekosea kabisa kulingana na Neno. Na hata hivyo, tunapaswa kwenda na Neno, si kwa yale Wasabato wanayosema,

ama si kwa yale Mprotestanti anayosema, ama Mkatoliki anavyosema. Ni yale Biblia isemayo.

87 Basi, sasa angalia.

> *Kwa maana ameinena siku ya saba mahali fulani hivi, . . .*

Sasa tutaweka kitu kama *hiki*, na kukiita hiki—hiki, "Raha ya Mungu," siku ya saba.

88 Sasa angalia, "Naye Mungu . . . " Sikilizeni Andiko hili sasa.

> *. . . Mungu alistarehe siku ya saba, akaziacha kazi zake zote.*

Mungu alikuwa na Sabato, na hiyo siku ya saba ilidumu miaka elfu moja, mfano wa ule Utawala wa Miaka Elfu Moja.

> *Kwa maana ameinena siku ya saba mahali fulani hivi,*
> *Mungu alistarehe . . . akaziacha kazi zake—zake zote;*

Kiwakilishi nafsi, "Kazi *Zake* zote." Alistarehe siku ya saba. Huyo ni Mungu.

> *Na hapa napo,* chini ya torati, *Kama wataingia rahani mwangu.*

89 Mungu alistarehe, kimwili, kwa kuwa alikuwa amezifanya mbingu na nchi katika siku sita, na katika siku ya saba Yeye alistarehe akaziacha kazi Zake zote. Alistarehe miaka elfu moja. Kwa kuwa Biblia ilisema, ya kwamba, "Siku moja duniani ni miaka elfu moja Mbinguni; miaka elfu moja Mbinguni; ni siku moja duniani." Ni wangapi wanaojua Maandiko yanasema hivyo katika Petro wa Pili? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Vema. "Mungu alistarehe kwenye siku ya saba. Naye alisema hivi mahali fulani."

90 Sasa sikilizeni kwa makini.

> *Kwa maana ameinena siku ya saba mahali fulani hivi,*
> Na *Mungu alistarehe . . . akaziacha kazi zake zote.*
>
> *Na hapa napo, torati, Hawataingia rahani mwangu.*

Aliwapa Wayahudi, walipokuwa njiani wakitoka kwenye nchi ya ahadi . . . ama kutoka Misri, kwenda nchi ya ahadi, sabato ya siku ya saba.

91 Sasa sikilizeni.

> *Basi, kwa kuwa neno hili limebaki kwamba wako watu watakaoingia humo, na wale waliohubiriwa habari ile zamani . . .*

Ile raha! Mungu aliwapa torati, nayo sabato ilikuwa ni amri ya nne.

> *. . . walikosa kuingia kwa sababu ya kuasi kwao, . . .*

92 Sasa angalia. Yeye anazungumza kuhusu torati, jinsi ambavyo waliingia, haikuchanganyika na imani. Hawakuishika.

Waliiadhimisha sabato katika kumbukumbu, kwamba walikuwa wakienda kwenye nchi ya sabato, wakapate raha ya milele kutokana na shida zao zote na wasiwasi wao wote, hakuna tena wasimamizi, hakuna tena siku za usiku wenye fadhaa. Walikuwa wakienda zao kwenye nchi waliyoahidiwa ya raha. Ilijaa maziwa na asali. Zabibu zilikuwa kubwa sana hivi kwamba watu wawili walibeba kishada kimoja mabegani mwao. Loo, ni nchi ya raha namna gani iliyobarikiwa! Lakini walishindwa kuipata wakati walipofika kule, kwa sababu ya kutokuamini kwao. Waligeuzwa kando, walipofikia tu maili arobaini toka pahali walipoondoka Misri, kufikia nchi ya ahadi. Nao walichukua muda wa miaka arobaini kufika kule, kwa sababu ya kutokuamini kwao. Mungu aliwapa nabii wao, akampa ishara Yake, akampa Nguzo ya Moto, akaonyesha ishara na maajabu, na kuwahubiri Injili. Nao wakatoka, wakaendea samaki na ile mikate, nao wakaanguka jangwani. "Na mizoga yao ikaangamia jangwani."

93 Yesu, pale kwenye chemchemi, alisema.

Wakasema, "Baba zetu walikula mana jangwani, kwa muda wa miaka arobaini."

94 Yeye akasema, "MIMI NDIMI kile Chakula cha Uzima kitokacho kwa Mungu Mbinguni. MIMI NDIMI Chakula cha Uzima. Musa hakuwapa Chakula hicho. Baba Yangu aliwapa Chakula hicho. NAMI ndimi Chakula kitokacho kwa Mungu kutoka Mbinguni. Mtu akikila Hiki, hatakufa kamwe." Hiyo ndiyo tofauti.

95 Sasa angalia. Wao walisema ya kwamba Yeye... "Waliunywea ule Mwamba uliokuwa nyikani, kwa muda wa miaka *kadhaa*."

96 Akasema, "MIMI NDIMI huo Mwamba." Jina Lake Takatifu lihimidiwe! "MIMI NDIMI huo Mwamba."

Yeye angewezaje kuwa huo Mwamba? Ule Mwamba ulikuwa ni Mwamba wa kiroho. Uliwafuata wana wa Israeli. Naye Musa alikuwa na fimbo mkononi mwake, ambayo ilikuwa ni fimbo ya hukumu ya Mungu. Ndipo Mungu akamwambia aupige ule Mwamba, naye akaupiga huo Mwamba. Basi alipofanya hivyo, maji yakatoka mwambani. Naye Kristo alikuwa ndiye ule Mwamba, na hukumu ya adhabu ya Mungu ya dhambi iliangukia juu Yake. "Mungu alisababisha kuweka juu Yake uovu wetu sote," na uovu huo ukaupasua moyo Wake. Na kutoka moyoni mwake kulimiminika Roho Mtakatifu, kama mito ya maji, kwa watu wanaopotea, watu wanaokufa.

"MIMI NDIMI ule Mwamba uliokuwa nyikani."

"Mbona," yeye alisema, "Hivi unataka kusema... "

97 Yeye akasema, "Musa, yeye aliyewaambia jambo hilo, alitamani kuiona siku Yangu. Naye aliiona kwa sehemu."

98 Akasema, "Sasa, unataka kutwambia ya kwamba Wewe u mkuu kuliko Musa? Ya kwamba umemwona Musa? Na Musa alikuwa amekufa miaka mia nane iliyopita." Kasema, "Sasa tunajua ya kwamba Wewe una pepo," kwa maneno mengine, "kichaa. Tunajua ya kwamba una kichaa."

99 Akasema, "Ibrahimu asijakuwako, MIMI NIKO. Mimi nilikuwa Ndiye YULE MIMI NIKO MKUU aliyekuwa kwenye kijiti kilichowaka moto. Mimi Ndimi ule Moto uliokuwa kwenye kijiti kilichowaka moto. Mimi Ndimi yule Malaika aliyekwenda mbele zao." Tena akasema, "Ninatoka kwa Mungu, na ninarudi kwa Mungu." Naye alitoka kwa Mungu, akafanyika mwili na kukaa kwetu; akarudi kwenye Nguzo ile ile ya Moto.

Naye yuko hapa, usiku wa leo, baada ya miaka elfu mbili, "yeye yule jana, leo, na hata milele," akifanya jambo lile lile, akiwaongoza watoto Wake waliobarikiwa.

100 Na wengi wanakuja. . .ndani kwa ajili ya kutokuamini. Sasa, yeye alisema, "Aliweka siku fulani," siku Mungu alipomaliza kazi Yake. Ndipo, "Aliweka 'siku nyingine,' na kwa namna hii, kwamba kama wataisikia, kama watakuja, wale wanaoadhimisha hizo sabato, wanapitia kwenye miandamo ya miezi na kadhalika." Huko ndiko hao ndugu Wasabato wanakojaribu kukurudisha.

101 Sasa hebu na tuendelee kusoma. Angalia.

> *Basi, kwa kuwa. . .kwamba wako watu watakaoingia humo, na wale waliohubiriwa habari ile zamani walikosa kuingia kwa sababu ya kuasi kwao,*

102 Sasa, kifungu cha 7. Loo, jamani! Ninasema, Maandiko yamevuviwa kihisabati. Ninasema, Maandiko yamevuviwa, na kwa kila njia, yamevuviwa. Hisabati za Biblia ni kamilifu.

103 Je! uligundua Marekani hii ni namba kumi na tatu katika kila kitu ifanyacho? Je! unajua ilianzishwa kama koloni kumi na tatu? Je! unajua bendera ile ilikuwa na nyota kumi na tatu ndani yake kwanza? Je! unajua kila kitu ambacho Marekani inafanya kiko kwenye namba kumi na tatu? Je! ulijua inajitokeza katika Biblia katika Ufunuo kumi na tatu? Hakika inajitokeza. Maskini Yule mnyama mdogo, yule mwana-kondoo aliyetokea kwenye maji, si kutoka katikati ya umati na halaiki ya watu, . . . si kutoka katika maji, bali kutoka katika nchi ambayo haina watu. Alikuwa na pembe mbili ndogo: mamlaka ya kiserikali na mamlaka ya kidini. Naye alikuwa ni mwana-kondoo: uhuru wa dini. Na baada ya kitambo kidogo, walienda pamoja naye akanena kama yule joka, na kutumia mamlaka yote ambayo Rumi ilitumia kabla yake. Hilo linakuja kwenye taifa letu. Hebu lizingatieni hilo. Liangalieni kwenye Muungano wa Makanisa na Katoliki wakiungana pamoja. Angalieni yale yanayotukia.

104 Watu wanaoifuata Nguzo ya Moto hakika watakuwa na wakati mgumu, bali wako tayari kwa ajili ya kuhamishwa

wakati huo, hiyo ni kweli, tayari tu kwenda. "Kwa kuwa Mwana-Kondoo aliwashinda," Biblia ilisema, "na hao waliomfuata, kwa kuwa waliitwa waliochaguliwa na waaminifu, Wateule wa Mungu." Hebu tusiuendee unabii huo sasa, tuweze kufuatilia hili.

105 Sikilizeni kwa makini, mlango wa 7, ninii . . . Ninamaanisha mlango wa 4, kifungu cha 7. Saba ni namba ya kumalizia. Tatu ni namba ya Uzima. Saba ni namba ya kumalizia, na hii inaleta sabato kamilifu.

"Na tena," kumbukeni, yeye alinena, "Mungu," kwa njia hii. Kisha alinena juu ya "torati," kwa njia hii. Na kisha, tena, "Aliweka siku fulani," siku ya tatu, mara ya tatu.

> Aliweka *tena siku fulani, akisema katika Daudi baada ya muda mwingi namna hii, Leo; kama ilivyonenwa tangu zamani, Leo, baada ya muda mwingi namna hii, kama ilivyonenwa tangu zamani, kama ninyi mtaisikia sauti yake; msifanye migumu* moyo wenu.
>
> Angalia, *maana kama Yesu angaliwapa raha* (sabato), *asingaliinena siku nyingine baadaye.*

Vipindi vya wakati hubadilika na Yesu Kristo: kutoka kwenye torati kuingia neema, kutoka matendo ya sheria kuingia kwenye neema, kutoka kwenye kitu fulani unachofanya kuingia kwenye kitu alichofanya Mungu, juu ya stahili ya matendo yako ama juu ya ustahili Wake. Ilibadilika.

106 Wakati Musa alipotoka jangwani, akiwa na torati, alisema, "Usizini. Usiibe. Usiue. Itakase siku ya sabato." Wakati Yesu alipotoka jangwani . . . Musa alipokuja, Ibilisi alimjaribu. Mara Ibilisi alipomjaribu, alimsikiliza. Musa alikuwa na sehemu fulani dhaifu. Ni wangapi wanaojua ilikuwa ni nini? Hasira. Na mara alipowaona wanaabudu ndama wa dhahabu, alitupa chini zile amri na kuzivunja, akikuonyesha ya kwamba ukuhani utavunjwa. Ndipo Mungu akampa hizo tena.

107 Lakini wakati Yesu alipotoka nyikani, siku arobaini za kufunga, aliona njaa, sehemu dhaifu pekee aliyokuwa nayo. Ndipo Ibilisi akamjia na kusema, "Ukiwa Ndiwe Mwana wa Mungu, yageuze mawe haya yawe mkate. Fanya muujiza hapa. Hebu nikuone ukiufanya, nami nitakuamini."

108 Yesu akasema, "Imeandikwa, 'Mtu hataishi kwa mkate tu, bali kwa kila Neno litokalo katika kinywa cha Mungu.'" Yeye alijua hakukutana na Musa pale, kwa maana alienda kwenye Neno.

109 Akamchukua akampeleka kwenye kinara, hekalu, kasema, "Ukiwa Ndiwe Mwana wa Mungu, jitupe chini." Naye *akapaka*, si ati alinukuu, bali aliyapaka Maandiko. Kasema, "Imeandikwa, 'Atakuagizia Malaika, wakulinde, kuhusu,

usije wakati wowote ukajikwaa mguu Wako katika jiwe. Atakuchukua.'"

110 Ndipo Yesu akaenda moja kwa moja kwenye Neno, na kumkaripia.

111 Akamchukua akampandisha juu ya mlima na kumwonyesha Marekani na Ujerumani na Uswisi, na mataifa yote ya ulimwengu, yatakayokuwako, kasema, "Yote ni yangu. Ninayafanyia lolote nipendalo." Si ajabu tuna vita na machafuko. Kasema, "Nayafanyia . . . " Si ajabu wanawake huvaa . . . na hawashikwi, na sheria. Yote yanatawaliwa na Ibilisi. Hivyo ndivyo Biblia ilivyosema. Shetani akasema, "Ni yangu. Ninayafanyia chochote nipendacho." Kasema, "Ikiwa utaniabudu, nitakufanya mfalme kama nilivyo mimi."

112 Yesu akasema, "Imeandikwa, 'Utamwabudu Bwana Mungu wako peke yake, utamtumikia.' Rudi nyuma Yangu, Shetani."

Kwa nini? Yesu alijua ya kwamba atayarithi katika Utawala huu mkuu wa Miaka Elfu Moja, wakati Ufalme Wake utakapokuja. "Mapenzi Yako yatimizwe duniani kama huko Mbinguni." Hakutakuwa na kuvaliwa kwa kaptura tena. Hakutakuwa na kunywa pombe tena. Hakutakuwa na tamaa mbaya tena. Hakutakuwa na uzinzi tena. Hakutakuwa na mauti tena. Hakutakuwa na huzuni tena. Yeye atakuwa mrithi wa kila taifa. Ni yake. Hiyo ni kweli. Ni Yake, Naye atayarithi. Lakini Shetani anayo kwa kipindi cha wakati, hiyo ni kusema, siku tunazoishi.

113 "Lakini ameweka siku, akisema, 'Leo, baada ya muda mwingi namna hii.' Na kasema, 'Msifanye migumu mioyo yenu.'"

*Maana kama Yesu angaliwapa raha, asingaliinena siku nyingine baadaye.*

114 Ndugu yangu Msabato, angalia jambo Hilo. Paulo hapa, alisema. Na Paulo alisema, katika Wagalatia 1:8, kama mnaandika maandiko, Wagalatia 1:8, "Kama Malaika kutoka Mbinguni akija na kuwahubiri injili nyingine yoyote isipokuwa Hii ambayo nimewahubiri, na alaaniwe." Paulo alisema, "Kama Yesu angaliwapa siku ya Raha . . . "

115 Angalia, wakati aliposhuka kutoka mlimani. Ndipo alishuka. Alikuwa amemshinda Ibilisi. Alikuwa ametiwa mafuta, akiwa tayari kwa huduma Yake. Akasema, "Mmewasikia wakisema, watu wa kale, 'Usiue,' bali Mimi nawaambieni ya kwamba kila amwoneaye ndugu yake hasira, bila sababu, amekwisha ua. Mmewasikia wakisema, watu wa kale," siku hii, hao washika-sabato. "Mmewasikia wakisema, huko nyuma zamani za kale chini ya torati, 'Usizini; ilipaswa mtu awe kwenye tendo lenyewe, kuwa na hatia.' Bali Mimi ninawaambieni, ya kwamba kila mtu amtazamaye mwanamke kwa kumtamani, amekwisha kuzini naye moyoni mwake.

Tofauti! Aliruka moja kwa moja hiyo amri ya nne. Lakini je! yeye aliwapa Raha?

116 Hebu na tuone alilosema. "Daudi alisema, 'Baada ya muda mwingi namna hii,' Raha kamilifu ingekuja. 'Mungu aliziacha kazi Zake, kwenye siku ya saba.' Mungu aliibariki siku ya saba, na akawapa hiyo Wayahudi huko jangwani, kwa jinsi hii. Waliingia...ndani kwa sababu ya kutokuamini, maana hilo Neno halikuchanganywa na imani. Na tena, Yeye aliiweka siku fulani, akisema katika Daudi, 'Baada ya muda mwingi namna hii.'"

Mamia ya miaka baada ya Daudi kufa, Mwana wa Daudi angeinuka, ambaye ni Yesu, "Na kama mtaisikia Sauti Yangu, msifanye migumu mioyo yenu." Mungu atasema na moyo.

117 Sasa angalia, kwa kifungu cha 9 sasa, kwenu ninyi mnaosoma. "Yesu angaliwapa raha," kifungu cha 8, "Angeninii...asingaliinena siku nyingine."

118 Kama Sabato ilipaswa kuwako, kama Jumapili ilipaswa kuadhimishwa, basi Yeye angalinena habari zake. Kama angalisema, "Sasa hakuna Sabato tena, hakuna tena kuadhimishwa kwa siku ya saba, ile ninayowataka mwadhimishe ni Jumapili," Yeye angaliisema. Paulo alisema alifanya hivyo. Yeye angalisema, "Nyote abuduni Jumapili. Hiyo ndiyo itakayokuwa raha." Vema, kama angaliwataka waadhimishe sabato, yeye angalisema, "Endeleeni tu kuadhimisha siku ya saba. Lakini sasa ninawataka mwadhimishe Jumapili, siku ya nane." La. Yeye kamwe hakusema jambo hilo.

119 Yeye alisema, "Kama Yesu angaliwapa siku fulani, si angalinena habari zake?"

120 Sasa kifungu cha 9. Iweni tayari.

> *Basi, imesalia raha ya sabato kwa watu wa Mungu,* kuadhimisha sabato *kwa watu wa Mungu.*
>
> *Kwa maana yeye aliyeingia katika raha yake* (ya Kristo), *amestarehe mwenyewe katika kazi yake, kama vile Mungu alivyostarehe katika kazi zake,* siku ya sabato.

121 Unaona jambo hilo? Sasa hebu na tuchukue Maandiko machache na kuliunga hili mkono. Sawa. Mungu alipoufanya ulimwengu katika siku sita, Yeye alistarehe siku ya saba, wala hakufanya kazi tena. Jina la Bwana litukuzwe. Aliujenga ulimwengu, akaweka viumbe humo, kisha akaenda kustarehe; wala hakurudi tena, kuujenga ulimwengu mwingine wowote. Alimaliza kazi hizo, kisha akaenda kustarehe. Sasa, kwenye... Halafu, baada miaka hiyo elfu moja, ndipo dhambi ikaingia; ndipo Kristo akawakilishwa, Mwana-Kondoo aliwakilishwa.

Sasa, Wayahudi walipewa hii kama kivuli cha Raha ya siku ya saba.

> Sasa, *aweka tena siku fulani, akisema katika Daudi baada ya muda mwingi namna hii,* kuna raha nyingine inakuja.

122 Sasa hiyo Raha ni nini? Fungueni pamoja nami katika Mathayo, mlango wa 11, na sehemu ya mwisho ya mlango wa 11 wa Mathayo Mtakatifu. Hapo ndipo Yesu alipomaliza mahubiri Yake kule mlimani, nanyi mtaona vile alivyosema.

123 Yeye alisema, "Kila mtu amtazamaye mwanamke, kwa kumtamani, amezini naye tayari moyoni mwake. Kila amwoneaye ndugu yake hasira, bila sababu, amemwua ndugu huyo." Mambo haya yote, wala Yeye kamwe hakugusa hiyo amri ya nne, hiyo sabato.

124 Sasa Yeye anamalizia. Na Sabato ni hiyo ahadi kuu ya Mungu. Ni Raha. Sasa, sasa angalia hapa, wakati alipomaliza zile heri. Hapa Yeye anasema, kifungu cha 27 cha mlango wa 11 wa Mathayo Mtakatifu. Pale, Yeye alipokuwa akifundisha zile heri katika mlango wa 5.

> *"Nimekabidhiwa vyote mkononi mwangu, na Baba yangu; wala hakuna amjuaye Mwana, ila Baba;. . .*

Unaona, huwezi kumjua mmoja bila kumjua huyo mwingine, maana Yeye alikuwa ni Baba aliyedhihirishwa katika mwili.

> *. . .wala hakuna amjuaye Baba, ila Mwana,. . .*

125 Inaonekana kana kwamba watu wangeweza kuona jambo Hilo wala wasibishane. Hakika. Mungu si Watu watatu. Kama Yeye ni Miungu watatu, basi sisi ni makafiri. Yupi ni Mungu? Hao, wote watatu, ni Mungu mmoja, ni ofisi tatu za Mungu yeye yule. Alikuwa ndiye Baba, katika umbo la Roho Mtakatifu, katika ile Nguzo ya Moto kule jangwani. Alikuwa ni Mwana, wakati alipoitumia ofisi ya Uwana. "Bado kitambo kidogo na ulimwengu hautaniona tena; nitaenda zangu. Nitakuja tena na kuwa pamoja nanyi, hata ndani yenu, hata ukamilifu wa dahari." Unaona? Yeye ni Ubaba, Uwana, na Roho Mtakatifu, pia. Yote ni Mungu yeye yule akifanya kazi katika ofisi tatu mbalimbali: Ubaba, Uwana, Roho Mtakatifu. Kamwe. . .

Yohana wa Kwanza 5:7 ilisema, "Wako watatu washuhudiao Mbinguni: Baba, Mwana, Roho Mtakatifu. Watatu hawa ni Mmoja."

126 Tomaso akamwambia, "Bwana, utuonyeshe Baba. Hilo litamtosha."

127 Akasema, "Nimekuwa pamoja nanyi muda mrefu hivi, wala hunijui Mimi?" Kasema, "Unaponiona Mimi, umemwona Baba. Na kwa nini kusema, 'Utuonyeshe Baba'?"

128 Sasa, wa Umoja walilichukua, kundi la watu wa umoja, na kujaribu kufanya Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu, ofisi moja tu na mahali pamoja, na kama kidole chako, kimoja. Hilo ni kosa. Mungu asingeweza . . . Yesu asingeweza kuwa baba wa Yeye mwenyewe. Kama alikuwa hivyo, basi alikuwa ninii . . . Vema, angewezaje kuwa baba wa Yeye mwenyewe?

129 Na kama Mungu ni mwanadamu, mbali na Roho Mtakatifu, alikuwa na baba wawili. Kwa kuwa Biblia ilisema, ya kwamba, "Roho Mtakatifu alimtia Mariamu uvuli naye akapata mimba, na," Biblia ilisema, katika Mathayo 1:18, ya kwamba, "mimba yake ni kwa uweza wa Roho Mtakatifu." Basi baba Yake ni yupi, Roho Mtakatifu ama Mungu? Wote wawili, Roho yeye yule, la sivyo Yeye alizaliwa kiharamu na roho mbili.

Hilo ni fundisho la sharti la Katoliki, wala kamwe halikuwa fundisho la Biblia. Martin Luther alitoka, pamoja na Ukatoliki mwingine mwingi ulioko katika kanisa la Kilutheri. Wesley alifuata akiwa na jambo hilo. Na lingali linaendelea, bali ni kosa. Si Kweli. Kamwe halikuwa, kamwe halikuwa ni Fundisho la Biblia. Kamwe halijakuwa ni amri ya Mungu katika Biblia, kufundisha Miungu watatu.

Kuna Mungu mmoja. Yesu alisema, "Sikia, ee Israeli, Mimi ni Bwana Mungu wako, Mungu mmoja," si Miungu watatu.

130 Huko Afrika, wanabatiza mara moja kwa Baba, mara moja kwa Mwana, na mara moja kwa Roho Mtakatifu. Na halafu maskini Myahudi anakuja, anasema, "Ni yupi kati yao ni Mungu wenu? Ni yupi, Baba, Mwana, ama Roho Mtakatifu?" Hao, wote watatu, ni Mmoja. Biblia ilisema hao ni Mmoja.

131 Yesu alikuwa ni nyumba alimoishi Mungu. Biblia ilisema hivyo, ya kwamba, Timotheo wa Kwanza 3:16, "Bila shaka," yaani, "ubishi, siri ya utauwa ni kuu. Kwa kuwa Mungu alidhihirishwa katika mwili, akaonekana na Malaika, akachukuliwa juu . . . akahubiriwa, akaaminiwa, na akapokelewa juu katika Utukufu." Mungu alipokelewa juu katika Utukufu. Biblia ilisema, "Ataitwa Jina Lake *Imanueli*, ambalo fasiri yake ni, 'Mungu pamoja nasi.'" Biblia ilisema, ya kwamba, "Yesu, ndani Yake mlikaa utimilifu wa Uungu kwa jinsi ya mwili."

132 Kama tulivyokuwa nalo hivi majuzi usiku: Mungu, hapo mwanzo, alikuwa ni Roho. Na halafu, kutoka kwa Mungu, kukatoka Logos, ama thiofani, ambayo ilikuwa ni umbo la mwanadamu, aliyeitwa Mwana wa Mungu, alipodhihirishwa kabla. Alikuja duniani, katika mwili wa nyama; hata kabla hajakuja katika Yesu Kristo. Sasa hebu meza hilo mara moja, ndugu. Nitakuthibitishia.

133 Wakati, wakati Musa alipomwona. Yeye alisema, "Hebu nione umbo Lako, Bwana." Ndipo Mungu akamficha kwenye mwamba. Na wakati alipopita hapo alipokuwa, yeye alisema,

"Lilikuwa ni mgongo wa mwanadamu." Huo ulikuwa ni ile thiofani. Hiyo ni kweli kabisa.

Halafu, huo thiofani ilibidi ufanyike mwili. Si Mtu mwingine, bali ni Mtu yule yule ambaye ilibidi afanyike mwili, apate kung'oa mwiba wa mauti.

Kama vile nyuki wakati anapochoma, yeye huacha mwiba. Wala yeye kamwe hakuuacha huo . . . Yeye angeweza kuuchoma mwili wa mwanadamu kwa maana huo ni dhambi. Lakini, ndugu, wakati alipoudunga huo mwili wa Imanueli, alipoteza mwiba wake. Naam, bwana. Anaweza kuvuma bali hana mwiba tena.

134 Si ajabu, Paulo, walipoenda kukikata kichwa chake, yeye alisema, "Ee mauti, u wapi uchungu wako? Unaweza kuvuma na kunguruma kadiri utakavyo. Kaburi, u wapi ushindi wako? Lakini Mungu na ashukuriwe atupaye ushindi kwa Yesu Kristo." Haya basi.

Ilimhitaji Mungu Mwenyewe kufanya jambo hilo. Alikuja na akadhihirishwa katika mwili. Akarudi katika Roho.

135 Unasema, "Ndugu Branham, hujatwambia, bado, ni wakati gani Mungu alipofanyika mwili kabla hajakuja katika Kristo."

Wakati Ibrahimu alipokuwa ameketi ndani ya hema lake, siku moja, walikuja Malaika wawili pamoja na Mungu, wakimwendea, katika miili ya kibinadamu. Walikuwa na mavumbi kwenye nguo zao na walikuwa wamechoka, nao wakaketi chini. Ndipo Ibrahimu akatoka akaenda akamtwaa ndama toka kwa ng'ombe, akamchinja. Akaikatakata katika vipande vya nyama ya mbavu. Akatoka na akachukua . . . akamwagiza Sara achukue unga na auchekeche, na akafanye mikate midogo. Kisha akachukua siagi kutoka kwa ng'ombe huyo, na akatengeneza mtindi. Akachukua hicho pale na akawaandalia, naye Mungu akakila.

136 Haleluya! Hiyo ndiyo sababu, "Imani yangu inakutumainia, Ewe Mwana-Kondoo wa Kalvari."

137 Unafikiri hilo ni jambo kubwa kwa Mungu? Mungu, Ambaye alifanya potashi yote na kalisi, na kila kitu duniani, alishuka akaja kumzuru Ibrahimu. Akasema, "Unafikiri nitakuficha, kwa kuwa wewe ni mrithi wa dunia?" Amina. "Sitakuficha." Mungu alichukua tu . . .

138 Sisi tumeumbwa kutokana na elementi kumi na sita. Yeye alichukua tu potashi kidogo, na kalisi kidogo, na petroli kidogo, na nurulimwengu kidogo, kisha "Whiu!" "Ingia ndani ya huo, Gabrieli," mwili!

139 "Whiu!" "Ingia katika huo, Pakanga." Akaingia ndani yake.

Malaika wawili, kutoka Mbinguni!

140 Mungu alinyosha mkono akachukua konzi yake, "Whiu," akaingia ndani yake, Yeye Mwenyewe. Akashuka, naye aliona njaa. Atukuzwe! Na hilo je! enyi ndugu Wasabato ambao hamtakula nyama? Tutaingilia jambo hilo, baada ya kitambo kidogo. Mungu Mwenyezi, Yehova, chunguza kama Jina lilo hilo halijatafsiriwa kwamba ni yeye Yule kwenye kijiti kilichowaka moto! Haleluya!

Na ndipo alisimama duniani, akasema, "Ibrahimu asijakuwako, MIMI NIKO, yeye yule kwenye kijiti kilichowaka moto." Hiyo ni kweli, Elohimu, angalia kama si yeye yule. Ndiye aliyekuwa kwenye kijiti kilichowaka moto.

141 Yeye alikuwa Ndiye hapa mbele za Ibrahimu, katika mwili wa nyama, aliyekula nyama ya ndama, na akanywa maziwa kutoka kwa ng'ombe, na akala siagi kwenye mkate. Jina Takatifu la Mungu litukuzwe! Akaenda moja kwa moja kule na kusema, "Sitaacha . . . "

Naye alikuwa amegeuza mgongo Wake. Akasema, "Ibrahimu, nitakuzuru, nawe utamzaa huyo mtoto. Una umri wa miaka mia moja sasa, naye Sara ana tisini." Naye Sara, huko hemani, akafanya, akacheka. Akasema, "Ni kitu gani kilichomfanya Sara kucheka?" Nyuma Yake; hema ikiwa kati yao.

142 Ibrahimu akasema, "Sara, je! ulicheka?"

143 "La, sikucheka kamwe."

144 Akasema, "Ndiyo, ulicheka." Ni telepathia ya aina gani hiyo? Kulikuwa ni kusoma mawazo kwa jinsi gani huko?

Yeye anafanya jambo lilo hilo siku hizi. Yeye ni Yehova-yire, Yehova-rafa, yeye yule jana, leo, na hata milele. Hashindwi kamwe.

145 Mwangalie. Huyo hapo amesimama. Akatoka moja kwa moja akaenda na kuzungumza na Ibrahimu; kisha akatoweka, mbele zake. Ndipo huyo mzee wetu mashuhuri Ibrahimu akasema "alizungumza na Mungu uso kwa uso, Elohimu," Mungu yule yule. Mnalipata? Wala si watu watatu, ndugu. Ofisi tatu za Mtu yule yule.

146 Hapo mwanzo alikuwa vivyo hivyo, Yeye alikuwa ni yule Roho mkuu, Chemchemi ambamo ukweli wote, upendo wote, amani yote. Kila kitu kilichokuwa kisafi kilikuwa katika Chemchemi hii. Ilianza kufanyiza mwili, thiofani, aina ya mwili tunaouendea. Si mwili uliotukuzwa, bali ni kama mwili wa malaika; una sura, umbo.

147 Kila ninapoona mti, ninafikiri, "Ule mti ni negativu. Kuna ulio halisi mahali fulani." Huo mti ulifanyizwa kutokana na kitu fulani. Akili fulani iliufanya. Na yote dunia hii inachofanya ni kuakisi ya Kimbinguni. Biblia ilisema hivyo. Na kama kuna mti

hapa ambao hauna budi kuangamia, kuna mmoja Utukufuni ambao hautaangamia.

148 Nikimwona mtu, ninawaona maskini mume na mke vijana wanaopendeza, mume na mke, wakishuka kwenda barabarani, wapenzi wanaopendana wako pamoja. Inaakisi nini? Jina la Bwana lihimidiwe! Kuna mke na mume Mbinguni ambao hawataangamia. "Kama maskani hii iliyo ya dunia hii ikiharibika, tuna moja inayongoja tayari, ile thiofania."

149 Ndipo unapata utatu: yule Roho mkuu, akikaa ndani ya Mwana, Yesu; Yesu akikaa ndani ya Kanisa. "Katika siku hiyo, mtajua ya kwamba Mimi niko ndani ya Baba, Baba yuko ndani Yangu, Nami ndani yenu." Yote aliyokuwa Mungu, Yeye aliyamimina katika Yesu; yote aliyokuwa Yesu, Yeye aliyamimina ndani ya Kanisa. Haya basi. "Mimi ndani ya Baba, Baba ndani Yangu; Mimi ndani yenu, nanyi ndani Yangu." Huo hapo ninii . . . Huo hapo ule Mwili.

150 Hiyo ndiyo shida iliyopo kwa kanisa. Wamefundishwa maskini fundisho duni la kitoto, dhaifu, la bibi kizee la namna fulani, kutangatanga na kufanya karamu za supu na tafrija za kadi. Si ajabu tuna lundo la machafuko tulilo nalo. Hatuhitaji vipindi vya watoto na milo midogomidogo ya supu. Tunachohitaji ni Injili kali ya kale, na watu wenye imani wakiwa na upanga unaotembezwa kule, na kutoa changamoto. Tunachohitaji siku hizi, si theolojia ya kitoto na nadharia fulani zilizotengenezwa na kundi fulani. Tunahitaji Injili kali iliyohubiriwa katika Nuru na Nguvu na madhihirisho ya Roho Mtakatifu.

151 Angalieni hapa sasa.

> *Kama alivyosema, yeye aliweka siku* nyingine, *akisema katika Daudi,*
>
> . . . *kama Yesu angaliwapa raha, asingaliinena siku nyingine baadaye.*
>
> *Bali imesalia raha ya sabato kwa watu wa Mungu.*
>
> *Kwa maana yeye aliyeingia katika raha yake, amestarehe mwenyewe katika kazi yake, kama vile Mungu alivyostarehe katika kazi zake.*

152 Sasa tutasoma wapi? Mathayo, ninii ya ishirini . . . Mlango wa 11, kifungu cha 27.

Vyote ambavyo Baba amenikabidhi, nimekabidhiwa *vyote na Baba yangu; hasa: wala hakuna amjuaye Mwana, ila Baba; vema, wala hakuna amjuaye Baba, ila Mwana, na ye yote ambaye Mwana apenda kumfunulia.*

153 Unaona, si kiasi gani unachojifunza, kiasi gani a—askofu anataka wewe ujue. Ni kiasi gani Mungu anachotaka ujue. Kama huwezi kuuona Ufunuo huu, usimwulize askofu. Mwulize

Mungu. Usimwulize mchungaji wako. Mwulize Mungu. "Mwana anamfunua Yeye," *Yeye*, kiwakilishi nafsi.

154 Sikilizeni. Hili litawashtusha. Hii hapa ile amri. Paulo aliyonena, "Kama angaliacha siku nyingine, angaliinena habari zake." Lakini hivi ndivyo alivyosema.

> *Njoni kwangu, ninyi nyote msumbukao na wenye kulemewa na mizigo, nami nitawapa* sabato, *raha.*
>
> *Jitieni nira yangu, mjifunze kwangu; kwa kuwa mimi ni mpole na mnyenyekevu moyoni, nanyi mtapata sabato nafsini mwenu.*
>
> *Kwa maana nira yangu ni laini, na* mizigo yangu ni myepesi.

155 Angalia aliyosema Paulo.

> *. . . kama Yesu angaliwapa raha, . . .* angaliinena *siku nyingine.*
>
> Bali *aliweka si . . . siku fulani, akisema katika Daudi baada ya muda mwingi namna hii, . . . mnapoisikia sauti yake, msifanye migumu* moyo wenu.
>
> "Ndipo imesalia . . . " Sikilizeni sasa, kifungu cha 9.
>
> *Basi, imesalia raha,* sabato fulani, *kwa watu wa Mungu.*
>
> *Kwa maana yeye,* mwanamume ama mwanamke, *aliyeingia katika raha yake . . .*
>
> "Njoni Kwangu, ninyi nyote msumbukao na wenye kulemewa na mizigo. Nitawapumzisha."
>
> *. . . amestarehe mwenyewe katika kazi yake, kama vile Mungu alivyostarehe katika kazi zake.*

156 Huenda ukawa umekuwa na umri wa miaka ishirini. Huenda umekuwa na umri wa miaka thelathini. Huenda umekuwa na umri wa miaka hamsini. Lakini dakika ile unapoisikia Sauti ya Mungu ikibisha moyoni mwako, usiufanye mgumu. Basi ingia . . . "Yeye ayasikiaye Maneno Yangu, amwaminiye Yeye aliyenipeleka Mimi, ana Uzima usio na mwisho, wa Milele, wala hataingia hukumuni bali amepita kutoka mautini kuingia Uzimani."

157 "Sema, Ndugu Branham, inakuwaje?" Unampata Roho Mtakatifu. Kristo anaingia ndani yako. Hiyo ni kweli?

158 Fungueni pamoja na mimi Isaya, mlango wa 28, na hebu tusome. Isaya, mlango wa 28, tuone vile nabii alivyosema juu ya jambo hilo. Mathayo . . . 28, tuanze na kifungu cha 8. Huu hapa utabiri wa siku za mwisho. Yatubidi kufunga sasa hivi.

> *Maana meza zote zitakuwa, zimejaa matapiko na . . . hapana mahali palipo safi.*

159 Hebu nisimame kwa dakika moja, kama vile Ernie alivyosema hivi majuzi usiku. Alikuwa akizungumza na mtu fulani. Ernie Fandler, ndugu huyu hapa kutoka Switzerland, alisema, "Nilisimama nikaliacha lipenye ndani."

160 Ninataka hili lipenye ndani.

> . . .*hapana mahali palipo safi.*
>
> *Maana meza zote* zitakuwa *zimejaa matapiko* . . .
>
> Na kama vile *mbwa* anavyoyaendea *matapiko yake* . . . *na nguruwe* . . .*katika kugaagaa* kwake, ndivyo watu wanavyorudi nyuma.

161 Kuna tatizo gani kwenu ninyi Wamethodisti? Hapo nyuma mlikuwa mna Nuru. Nini kilitukia? Mungu aliiondoa mkononi mwenu na kuwapa Wanazarayo.

Ilitukia nini kwenu ninyi Wanazarayo? Hapo nyuma mlikuwa na Nuru. Mungu aliitoa mikononi mwenu na akawapa Wapentekoste. Kweli. Ninyi kanisa la Mungu na ninyi watu wengine wa utakatifu, kwa kuwa mliikataa ile Nuru, mlijifanya madhehebu na kusema, "Hatutaamini zaidi ya *hili*," Mungu akaondoka akaendelea moja kwa moja na kuwaonyesha kuwa alikuwa na watu ambao wangemfuata.

162 Ilikuwaje kwenu ninyi Wapentekoste? Mlikuwa na Nuru. Mungu ameiondoa kwenu.

Nguzo ya Moto inasonga mbele. Kila wakati Nguzo ya Moto iliposonga mbele, Kanisa liliambatana Nayo.

Na wakati Luther alipounda madhehebu, kutoka katika kanisa Katoliki, kanisa lake mwenyewe, Nguzo ya Moto iliondoka moja kwa moja na Wesley akaambatana Nayo.

Wesley alianzisha utaratibu na kuunda madhehebu yake na hiyo Nguzo ya Moto ikahama na Wanazarayo wakaambatana Nayo.

Wanazarayo waliunda madhehebu, nalo kanisa la Mungu likaambatana Nayo; nao wakasema hawakuwa dhehebu, bali walikuwa madhehebu.

163 Basi ni kitu gani kilitukia? Jambo lililofuata lililotukia, Wapentekoste waliuona huo Moto, nao mara moja wakaenda. Nanyi mlifanya nini? Mkafanya fundisho la lugha, na kuliundia madhehebu, "Ilibidi kila mtu anene kwa lugha kabla hawajampokea Roho Mtakatifu," ndipo Mungu akahama moja kwa moja na akawaacha mmeketi mahali mlipo.

164 Ni nini kilichowapata ninyi wa Umoja? Mliuona ubatizo, Jina la Yesu. Mkauundia fundisho, kisha mkajitenga na mengine Yake, ndipo Mungu akaondoka mara moja na kuwaacha mmeketi pale. Kweli.

165 Ni nini kilichowapata ninyi Assembly of God, ile Halmashauri Kuu ya Kale? Mlijiundia madhehebu kutoka

katika makundi yenu, ndipo Mungu akaondoka moja kwa moja na kuwaacha mmeketi. Na sasa ninyi si kitu chochote ila kundi baridi, la wafuata sheria kama hao wengine walivyo.

Nayo Nguzo ya Moto inasonga mbele moja kwa moja. Haleluya!

> . . .*meza zote zimejaa matapiko* . . .

166 Angalia Meza ya Bwana. Mbona, hata kuna mahali fulani wanapokula mkate wa boflo uliochacha. Na mkate huo unapaswa kutengenezwa kwa mkate usiotiwa chachu. Nao wanawapa wenye dhambi, wavuta sigara, malaya, makahaba, mradi tu jina lao limeandikwa kwenye kitabu.

167 Ni ninyi Wabaptisti hata mnauita ushirika "maalum." Sasa, ninyi Wabaptisti mnawika kidogo, Mungu atawaondolea pembe yenu. Hilo ni kweli kabisa, hamtaweza kujivunia hizo. Ati ushirika "maalum," mnajitenga, mnaonekana kama ni watakatifu kuliko mlivyo.

Kumbukeni, hii ni maskani ya Kibaptisti. Hivyo ndivyo mnavyokuwa, mnapounda madhehebu yenu. "Loo," mnasema, "sisi si madhehebu." Ndio, ninyi ni dhehebu. Hakika, ndivyo mlivyo. Mnasema, "Sisi ni ushirika." Naam, kwa mtu yeyote anayeingia mlangoni na kufundisha jinsi tu mnavyoliamini, ni sawa. Lakini, mtu, ha—hamtamtupa nje, bali mtamfukuza kutoka katika udugu wenu. Hiyo ni kweli kabisa. Loo, mna njia ya kufanya jambo hilo. Vivyo hivyo Mungu anayo njia ya kufanya jambo hilo. Bali Kanisa la Mungu litasonga mbele. Nguzo ya Moto haitavumilia jambo hilo.

> . . .*meza zote zimejaa matapiko* . . .

168 Sasa sikilizeni. Sasa hili litawashangaza sana kwa muda kidogo tu. Sikilizeni. Nitasoma Neno. Huyu alikuwa ni nani? Nabii, Isaya.

> . . .*meza zote zimejaa matapiko* . . .kwa hiyo hapana kitu *safi,* ni hali tu ya unyang'au.

169 Njoo kanisani: wanawake wanachanja, wanakata nywele zao, wanavaa kaptura, wanatoka nje na kuwaona wanaume wakija barabarani; wanafyeka uwanja, wasichana wadogo wanataka kumsikia mtu akiwapigia mbija ya mbwa ama mbija ya mbweha, chochote kile ilicho, mwajua, "Whiu-whiu!" Loo, unafikiri wewe ni mzuri, sivyo?

170 Ninyi wanaume mnatembea barabarani, mkiwa na msokoto mdomoni mwenu, na ati ni shemasi kwenye halmashauri. Mnaonekana kama maksai wa Texas aliyeng'olewa pembe. Halafu unafikiri ya kwamba wewe ni mtu maarufu. Hiyo ni kweli kabisa. Si ajabu meza zote . . . Unaenda na kushiriki meza, na kujifanya kama wewe ni mtu maarufu, na unadanganya na kuiba na kusema uongo, juma zima. Una shida gani?

> . . .*meza zote zimejaa matapiko* . . .

171 "Loo, ninashiriki Meza ya Bwana. Hakika, tunafanya hilo kanisani mwetu. Yesu alisema atatufufua katika siku za mwisho kama tukishiriki Meza ya Bwana."

172 Lakini, "Yeye alaye na kunywa isivyostahili, hula na kunywa hukumu ya nafsi yake, kwa kutokuupambanua Mwili wa Bwana. Kwa sababu hiyo wako wengi kwenu walio hawawezi na dhaifu, na watu kadha wa kadha wamekufa," makanisa ya kale, ya kawaida, yaliyokufa. Roho wa Mungu amewatoka. Nguzo ya Moto haimo humo tena. Mnakana uponyaji wa Kiungu. Mnakataa ufufuo.

173 "Loo," mnasema, "loo, Yeye alifufuka toka kwa wafu, kihistoria." Vema, vipi kuhusu Yeye kuwa ni yeye yule leo, kama alifufuka toka kwa wafu? Unasema, "Loo, hiyo si kweli." Sasa, haya basi. Mnauchukua ufufuo jinsi unavyotaka, na Mungu anao jinsi anavyoutaka.

174 Lakini, jambo lenyewe ni kwamba, Biblia ilisema, yale tunayojua kwamba ni Kweli, ya kwamba Yeye angethibitisha Neno. "Na mambo haya nifanyayo ninyi nanyi mtafanya yayo hayo. Nami nitakuwa pamoja nanyi daima, hadi ukamilifu wa dahari." "Yesu Kristo yeye yule jana, leo, na hata milele." Hivyo ndivyo Neno lilivyosema.

175 Sasa sabato ni nini?

> *. . .meza zote zimejaa matapiko . . .hapana* mtu *aliye safi.*

> *Atamfundisha nani maarifa?*

Si maarifa ya kilimwengu; maarifa ya kiroho!

> *Atamfundisha nani maarifa? atamfahamisha nani habari hii?*

176 "Loo, Mungu atukuzwe, madhehebu yetu hayaamini jambo Hili. Wasingalivumilia Hilo." . . .sijali madhehebu yako yanaamini nini. Neno la Mungu linasema nini kuhusu jambo hilo? "Loo, vema, wachungaji wetu, unajua, wameelimika." Loo, hakika. Bila shaka, wana elimu kubwa sana, hata walimwacha Mungu nje yake. Hakika, kwa kuwa unaweza kuwaambia Neno nao watazunguka-zunguka na kusema, "Vema, siliamini tu jinsi hiyo." Loo, ewe kiumbe dondoadume wee! Hebu nikwambie.

177 Angalia hapa.

> *Atamfahamisha nani maarifa? Ni wale walioachishwa titi,* na *. . .wale walioachishwa maziwa, walioondolewa matitini.*

178 Hivi majuzi, jirani yangu alikuja. Akasema, "Billy, mchungaji fulani hapa mjini, maskini mtu mzuri sana uliyepata kumwona . . . " Kasema, "Mimi na mke wangu tulikuwa tumeketi tumevaa pajama zetu, yapata usiku wa manane, na maskini mchungaji huyo akaingia upesi na a—a—akanywa kahawa

pamoja nasi kisha akaondoka akaenda nyumbani kwa jirani mwingine, akapeana mkono nao. Walikuwa wakicheza mchezo mdogo wa karata, naye akaketi na kucheza karata pamoja nao." Kasema, "Loo, alikuwa ni maskini mtu mchangamfu sana uliyepata kuona." Kasema, "Loo, tunampenda. Tusingeweza kumwondosha kwa chochote kile."

179 Nilisimama pale kidogo, nikawazia, "Vema?"

180 Kasema, "Loo, hivi hudhani ya kwamba kila kanisa linahitaji mtu kama huyo?" Aha! Singeweza kujibu hilo. Akasema, "Kwenye jengo lingine maalumu," kasema, "walikuwa na jengo zuri sana. Mhudumu huyu pamoja na mkewe, watu wazuri sana, walitoka wakaenda wakawashughulikia watoto sana mpaka wakawa na shule ya—ya Biblia." Na akasema, "Walikuwa nao wengi sana, walipajaza tu mahali hapo na watoto." Kasema, "Jamani, anaweza kuwasimulia hao watoto wadogo kila namna ya hadithi."

181 Nikasema, "Hilo ni jambo zuri. Hilo ni zuri sana."

182 Nikarudi. Ndiyo kwanza nitoke Canada. Nikawazia, "Mimi hapa. Jamani! Watu. . .Nina shida gani? Mimi sifanyi jambo hilo." Nikaingia kwenye kuosha gari langu. Nikawazia, "Mungu, ninazeeka, nami ndiye huyu hapa. Nimepigana. Nimelia. Nimesihi. Na ninachopata ni kukufuru kukubwa."

183 Kitu chochote, hebu mtu fulani aseme jambo fulani baya kukuhusu wewe, "Loo, maskini mtakatifu anayejifingirisha," kitu kama hicho.

184 Niliwazia juu ya jambo hilo. Ndipo Sauti ikanijia, ikasema, "Hao watu ni sawa kama wanafanya hivyo, bali Mimi sikukuita kamwe ukafanye hivyo. Nilikuita uchukue Upanga na usimame pale kama Yoshua na kusai, ndugu. Si kujipumbaza na shirika fulani la kale ama shirika fulani la kanisa, bali simama msai Ibilisi. Usimame mstari wa mbele kweli iite kweli, na uongo uuite uongo. Hubiri Neno na uone ni nani aliye na imani ya kuliamini. Uliweke huko uwanjani."

185 Nikaendelea kuharakisha kushughulikia hilo gari, wakati wote, nikiosha. Nikasema, "Asante, Bwana. Asante, Bwana." Ndipo nikajisikia vizuri. "Ni sawa, Bwana, nitaushika kwa nguvu zaidi kidogo, nami ninataka kufa nikiwa nimeushika mkononi mwangu."

> . . .ninaweza *kumfahamisha nani habari hii?* (Sikiliza.)
>
> . . .*meza zote zimejaa matapiko*. . .
>
> . . .*wale walioachishwa maziwa, walioondolewa matitini.*

Sasa angalia.

*Kwa maana ni amri* kama *hiyo juu ya—juu ya amri, amri juu ya amri; kanuni juu ya kanuni; huku kidogo, na huku kidogo.*

*La, bali kwa midomo ya watu wageni, na kwa lugha nyingine* nitasema *na watu hawa;*

*Ambao ilinenwa, Hii ndiyo* sabato *yenu* ambapo *mtampa raha yeye aliyechoka; huku ndiko* kuburudika*; lakini hawakutaka kusikia.*

*Kwa sababu hiyo neno la* B*WANA* lilikuja *kwao, mtu fulani* alilihubiri, *amri juu ya amri,. . .juu ya amri; kanuni juu ya kanuni,. . .juu ya kanuni; huku kidogo, na huku kidogo; ili waende na kuanguka nyuma, na kuvunjwa, na kunaswa, na kuchukuliwa.*

186 Raha ni nini? Je! Raha ilikuja lini? Wakati watu waliponena kwa midomo ya watu wageni na kwa lugha nyingine. Lugha nyingine; hawakusema kitu. Waligugumiza. Hayo yalitukia lini? Kwenye siku ya Pentekoste, wakati Roho Mtakatifu alipokuja. Hiyo ndiyo hiyo Raha: Roho Mtakatifu. Yesu alisema, "Njoni Kwangu, ninyi nyote msumbukao na wenye kulemewa na mizigo, nami nitawapa Raha. Nitawapa Uzima, Uzima wa Milele," *Zoe*, Uzima wa Mungu Mwenyewe. Mungu atakuja ndani yako na kuwa sehemu yako. Atakuzaa na kukufanya mwana na binti.

187 Sasa angalia. Hiyo ilikuwa ndiyo raha ya tatu aliyowapa. Ya kwanza: Mungu aliipata, kutokana na kazi Yake. Ya pili: Israeli waliipokea, katika torati. Tatu: Kanisa liliipokea, kama sehemu ya Mungu.

188 Tatu ni namba ya uhai. Ni wangapi wanaojua jambo hilo? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Kila wakati unapoona tatu, ni uhai. Angalia, wakati Mungu alipoiumba nchi, katika siku ya tatu kulitokea uhai. Ni wangapi wanajua jambo hilo? ["Amina."] Siku ya tatu. Kulitokea uhai kwenye siku ya tatu ya uumbaji.

Utatu: Baba alikuwa juu ya watu, katika Nguzo ya Moto, Mwana alikuwa Mwanadamu, aliyezungumza na watu na kuwatayarisha; Roho Mtakatifu alikuwa ni hatua ya tatu, ambayo ilikuwa ni Roho Mtakatifu, Mungu ndani ya watu. Uzima! Baba, Mwana . . .

Raha, ya Mungu; raha, ya Israeli; na Raha, ya Kanisa, kuadhimisha sabato.

189 Kwa hiyo, kama hujawahi kumpokea Roho Mtakatifu, bado, hujaingia kamwe katika Raha ya Mungu. Haikubidi kusema, "Loo, nisingeweza. Ninataka kuvuta sigara. Ni—singeweza kabisa kufanya jambo hilo; mimi ni Mkristo. Kwa kweli sitaki kunywa pombe, bali mimi ni Mkristo. Siwezi kabisa, sitaki kunywa, bali hata hivyo ninapenda kunywa."

190 Kama ukiwatamani wanawake, kama ukifanya mambo haya yote mabaya, hujafikia kwenye kipindi hicho cha Raha bado. Hujaingia kamwe katika Raha yako.

191 Na ndipo unapoingia katika Raha hii, unaacha kufanya shughuli zako za kilimwengu, kama Mungu alivyoacha kufanya Zake. Kwa nini? Wewe ni sehemu ya Mungu. Unastarehe, Milele. Haya basi. Hiyo ndiyo Sabato. "Njoni Kwangu, ninyi nyote mliolemewa na mizigo mizito."

> Leo*, aweka . . . siku fulani, . . . katika Daudi baada ya muda mwingi namna hii, . . .* mtakapoisikia *sauti yake, msifanye migumu mioyo yenu.*

192 Neno moja tu ama mawili zaidi hapa sasa, tutafunga.

> *Kwa maana yeye ambaye ameingia katika raha* ya Kristo . . .
>
> Njoni kwangu, ninyi *nyote msumbukao na mizigo mizito . . .*
>
> . . . umestarehe *mwenyewe katika kazi* yako*, kama vile Mungu alivyostarehe katika kazi zake,* katika siku ya saba.

Huenda kwako kulikuwa kwenye mwaka wa thelathini, mwaka wa arobaini, mwaka wa tano, wowote ule. Umestarehe mwenyewe katika kazi zako, kama vile Mungu alivyostarehe katika kazi Zake, Milele. Hutaki tena mambo ya ulimwengu. Ulimwengu umekufa kwako.

193 Sasa, kifungu cha 11 sasa, kwa makini.

> *Basi, na tufanye bidii kuingia katika raha ile,* (si *hii*, si *hii*, bali *Hii*), *ili kwamba mtu ye yote asije akaanguka kwa mfano uo huo wa kuasi.*

194 Ni kitu gani? Nguzo ya Moto iko hapa. Malaika wa Bwana yuko pamoja nasi. Anafanya mambo yale yale aliyosema atafanya. Na watu kila mahali wanajikwaa, kusema, "Loo, vema, nadhani ni sawa. Hilo ni zuri sana. Loo, nadhani ni sawa." Iweni waangalifu msije mkaangukia katika mtego ule ule wa kuasi. Lichukue kwa moyo wako wote.

195 Angalia.

> *Maana Neno la Mungu* (si fundisho la kanisa) . . . *Neno la Mungu li hai, tena lina nguvu, . . . lina ukali kuliko upanga uwao wote ukatao kuwili,* (sikilizeni), likichoma *hata kuzigawanya nafsi na roho, . . . viungo na mafuta yaliyomo ndani yake; tena . . .* (sikilizeni), *li jepesi kuyatambua mawazo na makusudi ya moyo.*

Hilo ilikuwa ni nini? Roho Mtakatifu anaweza kuja na kusema, "Ulifanya jambo *fulani na fulani*. Na ulifanya *hivi* na *vile*. Una ugonjwa na aina *hii*, na *ile*. Kama utasahihisha jambo *hili*, utafanya *vile*." Unaona? Huyatambua mawazo.

196 Na watu wanasema, “Hicho ni kitu gani? Mbona, ni telepathia ya mawazo. Mbona, ni ninii . . . Yeye ni mpiga ramli.” Unaona ninalomaanisha? Ni ulimwengu ule ule mwovu wa kale, wa zinaa ambao haumjui Mungu.

197 “Ni jepesi, mawazo, lina nguvu kuliko upanga ukatao kuwili, tena huyatambua mawazo na makusudi ya moyo.”

Sasa, ni kitu gani kinachojua makusudi ya moyo? Mungu. Ulisema, “Vema, Biblia ilisema, ‘Neno la Mungu.’” Neno la Mungu ni Mungu.

> *Hapo mwanzo kulikuwako Neno, . . . Neno alikuwako kwa Mungu, naye Neno alikuwa Mungu.*
>
> *Naye Neno alifanyika mwili, akakaa kwetu, . . .*

198 Mungu huyatambua mawazo. Ibrahimu alikuwa amegeuza mgongo Wake, na—na vivyo hivyo Mungu alikuwa ameulekeza mgongo wake kwenye hema. Na Sara akacheka. Basi Mungu akageuka, kasema, “Ni kitu gani kilimfanya Sara acheke?” Huyatambua mawazo ya moyo! Ninataka hilo likolee kidogo.

199 Basi wakati huduma ya aina hiyo inapojitokeza, ambayo Mungu aliiahidi katika siku ya mwisho, ni kitu gani kilitokea? “Telepathia ya mawazo.”

200 Hivi hawakumwita Bwana, Mwenyewe, “Beelzebuli?” Alisema, “Kama wamemwita Bwana wa nyumba ‘Beelzebuli,’ ni zaidi sana vipi watawaita wanafunzi Wake?”

201 Ninawapenda. Inaonyesha ya kwamba ninyi mnapenda vya kutosha, hamna haja ya kuja kwenye jengo lililoyoyozwa kuisikiliza Injili. Mna njaa vya kutosha kuja mahali kama hapa. Mungu asingeturuhusu kujenga kitu chochote ila hiki. Tunaipenda ikikaa namna hii. Kibanda kidogo tu cha kale, bali hivyo ndivyo tunavyopapenda. Mungu haishi katika mambo ya kuvutia. Mungu anakaa katika unyenyekevu. Tanapapenda jinsi hii. Tuna furaha kuja, nanyi mnafuraha, pia, kuketi kwenye ninii—mahali kama hapa. Haidhuru pana joto jinsi gani, jinsi gani unavyotokwa na jasho katika suti yako mpya, nguo yako mpya, hilo halileti tofauti yoyote.

Mnasikiliza Uzima wa Milele, Neno la Mungu linalojua mawazo ya moyo wako. Ile Nguzo ya Moto iliyoning’inia juu ya wana wa Israeli, inaning’inia hapa usiku wa leo. Ningeweza kulipa hilo changamoto: hakuna mtu angeweza kusimama hapa chini ya nguvu za Roho Mtakatifu bila Mungu kumwangusha na kumwambia kile yeye alichokuwa. Hiyo ni kweli. Haya basi.

202 Ni kitu gani? Ni kitu gani? Ni Roho yeye yule aliyewaongoza Wana wa Israeli kwenda kwenye raha yao, nao walianguka kwa sababu ya kutokuamini. Msianguke. Hii ndiyo nafasi ya mwisho. Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu, Uzima unapitia hapo.

203 Kuhesabiwa haki, Martin Luther, bado ni utaratibu tu wa dini. Utakaso . . . Martin Luther, John Wesley; ubatizo wa Roho

Mtakatifu, Uzima. Kuhesabiwa haki, ni kuamini; kutakaswa, ni kusafishwa; Roho Mtakatifu, ni ujazo, Uzima. Si kupitia wakati wa Kilutheri; walikuwa na Huo katika mfano. Si kupitia katika wakati wa Wesley; walikuwa na Huo katika mfano. Bali huu ndio wakati ambapo Roho Mtakatifu anakuja, Mwenyewe.

204 Na endapo hujampokea, unaninii vipi, je! unawezaje kuamini miujiza? Hilo linamhitaji Mungu, ndani yako, kuamini. Unatenda kama Mungu. Unajua kama Mungu. Unafikiri kama Mungu. Biblia ilisema ya kwamba ninyi ni "miungu" wadogo. Yesu alisema hivyo. Kwa kuwa, wewe ni sehemu ya Mungu.

Ni jinsi vile vile tu mimi nilivyo Branham mdogo, na wewe ni yeyote awaye yule mdogo, na kwa sababu wazazi wako wanaitwa hivyo. Tabia uliyo nayo ni kwa sababu wazazi wako wako hivyo, maana ulizaliwa nao.

Na sababu ya wewe kumwamini Mungu, na kuamini miujiza, na ishara na maajabu, ni kwa sababu ninyi ni wana na binti za Mungu. Mnapokea Uzima. Uzima unakuja kwenye ya tatu. Vema.

205 Wakati Yesu alipopanda mlimani, kila mahali alikoenda, aliwachukua Petro, Yakobo, na Yohana, mashahidi watatu. Tatu ni namba ya Uzima. Mnalipata? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Upendo, furaha, amani.

206 Sasa, hebu na twende upesi sasa kwenye mwisho wa mlango huu, upesi, tunaposoma.

> *Maana Neno la Mungu li hai, lina nguvu* zaidi. . . kuliko *upanga ukatao kuwili,*. . .na kuyatambua hata *na makusudi ya moyo.*
>
> *Wala hakuna kiumbe kisichokuwa* wazi *mbele zake, lakini vitu vyote vi utupu na kufunuliwa machoni pake yeye aliye na mambo yetu.*

207 Ndugu, hakuna nzi angeweza kuketi kwenye nguzo pale, bila Yeye kujua jambo hilo. "Vitu vyote vi utupu." Ndugu, Yeye anajua kila kitu ulichowahi kufanya, kila wazo ulilopata kuwazia. Hivyo ndivyo Yeye alivyo. Tunamwamini hivyo.

Na Mungu anapoingia ndani yetu, na kutuweka ndani ya Kanisa, Yeye huweka karama na kadhalika katika Kanisa, kutumia Utu Wake. Kama Mungu ni Mungu ambaye hana kikomo jinsi hiyo, basi Yeye huwaponya wagonjwa. Anaweza kufufua wafu. Anaweza kuwatakasa wenye ukoma, kuwafanya vipofu waone. Anaweza kuonyesha maono. Anaweza kufanya kila aina ya mambo haya, akitenda kazi katika Kanisa Lake, kwa maana ni Mungu ndani yako. Hilo ndilo Kanisa.

208 Kanisa hilo linakuwaje Kanisa, kwa kujiunga Nalo? La, bwana. Kwa kupeana mikono? La, bwana. Kwa ubatizo wa maji? La, bwana. Kwa uanachama? La, bwana. Unalipataje? "Kwa

maana katika Roho mmoja sisi sote tulibatizwa kuwa Mwili mmoja." Haya basi.

209 Warumi 8:1.

> *Sasa basi, hakuna hukumu ya adhabu . . .*

"Hakuna hukumu ya adhabu ya kidunia." Hawawezi kukushtaki kwa jambo lolote.

> *Hakuna hukumu ya adhabu juu yao walio katika Kristo Yesu wasioenenda kwa kufuata mwili bali kwa Roho.*

210 Haya basi. Hivyo ndivyo unavyopaswa kupima Ukristo wako. Hiyo ndiyo jinsi ya kujua umeingia katika ile Raha, ulimwengu haukusumbui tena. Hakika. Unauona, unaondoka kwake. Una kitu kilicho bora zaidi cha kuwazia. Haya basi, "Hakuna hukumu ya adhabu." Hivyo ndivyo tunavyoingia katika ule Mwili.

211 Nawe umewekwa salama, "Milele." Biblia ilisema hivyo. Angalia hapa katika Waebrania, mlango wa 10. Yeye alisema:

> Kwa kuwa palipo na matoleo ya mafahali na dhabihu, liko *kumbukumbu* la dhambi *kila mwaka*.

> *Lakini mtu huyu, . . . kwa toleo moja . . .*

Jina Lake takatifu libarikiwe!

> *Maana kwa toleo moja amewakamilisha hata milele . . .*

212 Haleluya! Si kwa ufufuo ujao, bali *milele*. "Ya kale yamepita; na mambo yote yamekuwa mapya." Tunatembea katika Nuru, Nuru nzuri. Ndege wanaimba tofauti.

213 Nikiketi hapa, nikimwangalia maskini huyu mlevi sugu, yapata miaka mitano iliyopita, nadhani. Rosella, mwenye macho ya makengeza, akitembea huku na huko katika mitaa ya Chicago, amelewa, akiyumbayumba, akiingia katika kila namna ya dhambi iliyokuwako, amelewa na yuko katika kila kitu ambacho angaliweza kuingia. Ndipo usiku mmoja, Roho Mtakatifu, ambaye ni mwepesi na mwenye nguvu kuliko upanga ukatao kuwili, kasema, "Ewe mwanamke, wewe ni mlevi sugu." Haleluya! Kama huyo si Mungu yeye yule aliyekuwa kule nyuma, aliyejua Sara alicheka nyuma Yake, sijui Yeye ni nani.

214 Huko kwa wasikilizaji kwa maskini mwanamke mwingine. Yeye alienda akampata, na kumleta hapa ndani. Kasema, "Wewe ni mlevi sugu wa madawa ya kulevya." Jinsi Yeye anavyotambua nia ya mawazo!

215 Na wahudumu wakuu mashuhuri na wenye vyeo wameketi pale, walio na huduma ya uinjilisti ya ulimwengu mzima, huku wamekunja mikono yao nyuma yao, wamevaa fulana za mikono, walidhani hatukuwajua, kana kwamba wangaliweza kuketi chini ya mkutano kama huo na Mungu asifunue kwamba

walikuwa ni nani. Wameketi pale, wakionekana si watu wa aina hiyo, kana kwamba walikuwa ni kama watu wengine. Roho Mtakatifu aliwajua hao walikuwa ni akina nani. Nao wakaketi pale, mioyoni mwao, wakidhani ilikuwa ni telepathia ya mawazo. Hawajui zaidi juu ya Mungu kuliko Mhotentoti angejua juu ya hekaya za Wamisri. Hiyo ni kweli. Wanalijua kwa Andiko, bali si kwa Roho. "Andiko huua, bali Roho huhuisha." Hivyo ndivyo ilivyo. Hilo ni wazo la kufikiriwa. "Li jepesi, tena lina nguvu kuliko upanga ukatao kuwili, huyatambua mawazo na makusudi ya moyo."

216 Sikilizeni. Angalieni.

> *Wala hakuna kiumbe kisichokuwa wazi mbele zake, lakini vitu vyote vi utupu na kufunuliwa machoni pake . . . aliye na mambo yetu.*
>
> *Basi, iwapo tunaye kuhani mkuu . . .* (Sikilizeni sasa; kwenu ninyi wagonjwa) *. . . aliyeingia katika mbingu, Yesu, Mwana wa Mungu, na tuyashike sana maungamo yetu.*

217 "Tuyashike sana," hilo halimaanishi kuendelea tu kushuhudia. Kama huyaishi maisha hayo, wewe huyashiki sana; unaishi jambo la kinafiki. Unaninii . . . Afadhali ujitokeze wazi na kusema tu kwamba wewe ni mwenye dhambi na usahau jambo hilo. Usikiri kuwa Mkristo, huku unaishi kitu kingine; wewe u jiwe kubwa sana la kujikwaa ulimwengu ulilopata kuwa nalo. Kama wewe ni mwenye dhambi, kubali jambo hilo na, uendelee, jiweke sawa na Mungu. Kama wewe ni Mkristo, shika sana maungamo yako, kaa hapo.

218 Angalia jambo hili sasa. Ninataka kuingiza jambo hili kabla tu hatujaondoka.

> *Kwa maana hatuna kuhani mkuu asiyeweza kuchukuana nasi katika mambo yetu ya udhaifu; bali yeye alijaribiwa sawasawa na sisi katika mambo yote, bila kufanya dhambi.*

Sikilizeni.

> *Basi na tukikaribie kiti cha neema kwa ujasiri, ili tupewe rehema, na kupata neema ya kutusaidia wakati wa mahitaji.*

Jina la Mungu lihimidiwe.

219 Sikiliza, ewe Mbaptisti, Mpresbiteri, Mlutheri. Utaniuliza swali hili, "Ibrahimu alimwamini Mungu, na ikahesabiwa kwake kwamba ana haki." Ninajua. Hapo ndipo unapoelekea sikuzote. Hiyo ni kweli. "Mtu anaweza kufanya nini zaidi isipokuwa kumwamini Mungu?" Hiyo ni kweli kabisa. Hivyo tu ndivyo anavyoweza kufanya. Lakini wakati Mungu anapoitambua imani hiyo, Yeye anakupa Roho Mtakatifu.

220 "Sasa nifanye nini, Ndugu Branham? Je! inabidi nipige makelele?" Si lazima. "Je! inabidi ninene kwa lugha?" Si lazima. Unaweza kupiga makelele na kunena kwa lugha, yote mawili, na bado uishi ka—kama kafiri, na bado uwatamani wanawake. Unaweza bado uvute sigara na kunywa pombe, na chochote kile. Nimewaona watu wakinena kwa lugha, kisha waende moja kwa moja na kufanya jambo chafu sana nililowahi kuona. Nimewaona wakipiga makelele, na kulia machozi ya kinafiki, nao wangeweza kuiba chochote unachopata. Nimewaona wakitoka, na kila msichana anayepita barabarani, wanageuka. Uh-huh. Hiyo ni ishara moja nzuri ya kwamba hujampata. Hiyo ni kweli.

221 Lakini, ndugu, unapokuwa umepita toka mautini kuingia Uzimani, mambo hayo yote yanakufa, nawe ni kiumbe kipya katika Kristo Yesu. Kama ukiona kitu fulani kibaya, utakiombea, "Mungu mrehemu." Na ukiona vurugu, badala ya kwenda na kupiga domo, na kujaribu kulifanya liwe baya zaidi, utajaribu kumwendea mtu huyo na kulinyosha, na kulinyamazisha upesi sana. Huyo ni Roho wa Mungu ndani yako.

222 Ukifanya kosa? Unaweza kuyafanya. Kama ukifanya kosa, utalisahihisha upesi sana. "Usiache jua litue ukiwa bado umeshikilia hasira yako." Hivyo ndivyo unavyojua umepita toka mautini kuingia Uzimani, una upendo, amani, furaha, uvumilivu, wema, utu wema, saburi. Tunaye Kuhani Mkuu anayekaa Mbinguni, aliye tayari kutuombea tufanyapo maungamo yetu. Ni kitu gani? Ni wakati Yesu aliporudi kwenye Logos, ile Nguzo ya Moto iliyowaongoza wana wa Israeli, ameketi Uweponi mwa hizo chemchemi kuu za Nuru za upinde wa mvua zinazotokea wazi, zile Roho Saba kamilifu, Roho mkamilifu wa upendo.

223 Sasa angalia. Wa kwanza ni upendo *mkamilifu*, huo ni upendo wa Mungu, ulio msafi na usiogoshiwa. Wa pili, unaoingia mle, ni upendo wa *fileo*, huo ni upendo ulio nao kwa mke wako na watoto wako. Unaofuata, unaoshuka baada ya huo, ni upendo wa *tamaa mbaya*. Unaofuata ni upendo *mwovu*. Na unaendelea tu kushuka mpaka ukawa ni *uchafu*, unaendelea tu kupotoka, kupotoka.

224 Na kila kitu kilichokuwa na mwanzo, kina mwisho. Na hayo yote yataondolewa, wala hakutakuwa na kumbukumbu la hayo, hata kidogo, na kurudi moja kwa moja kwenye ule mkamilifu, siku moja. Na njia pekee . . . Huwezi kusimama hapa chini, nusu njia ya njia, na ufike *hapa* juu. Huna budi uwe ndani njia nzima, ukitumaini, ukipumzika kabisa katika wokovu ambao Yesu Kristo anakupa, kwa imani.

225 Kuna Roho wa uaminifu anayetoka kwa Mungu. Hiyo ndiyo chemchemi, chemchemi ya Mungu. Huo ni uaminifu. Nyingine

ni mtu huyo ambaye atafanya "tendo jema" kwa jirani yake. Nyingine ni jamaa huyo, "inakupasa umchunge." Nyingine ni jamaa ambaye, "ni mwizi." Nyingine ni jamaa ambaye, "ni mwuaji," jambazi. Unaona jinsi unavyopotoka, moja kwa moja kushuka chini? Lakini vitu hivyo vyote vinanena habari za kilicho halisi.

226 Hivyo ndivyo ninavyosema. Kila wakati unapomwona mtu ambaye. . . Unapowaona maskini mume na mke wakishuka kwenda barabarani, wapenzi, labda wana umri wa miaka themanini. Inanena tu kwamba huko Mbinguni kuna mke na mume vijana wanaowawakilisha, huko Mbinguni. "Kama maskani hii iliyo ya dunia hii ikiharibika, tuna moja Kule."

227 Ukiona mtu anayedanganya, anayeiba, anayesema uongo, kumbuka tu, sehemu yake inangoja jehanamu, kwa ajili yake, mahali pake ambapo atateswa Mbele za Mungu na Malaika watakatifu, kwa moto na kiberiti. Atateswa kule. Si milele, hawezi kuteswa milele, milele haimaanishi zote, nyakati zote. Milele ni daima, Milele ni . . . haina mwanzo wala mwisho. Lakini *daima* ni "kipindi cha wakati." Biblia ilisema, "Milele na," kiunganisho, "milele." Yona alisema alikuwa katika tumbo la nyangumi "daima." Ni kipindi cha wakati.

228 Lakini, angalia, kuna Uzima mmoja tu wa Milele, na huo ni Mungu. Na kama utateswa milele, wala huwezi kufa, una Uzima wa Milele. Huwezi kuteswa milele. . . Huenda ukateswa kwa miaka milioni mia moja, Uweponi mwa Mungu na Malaika watakatifu, kwa moto na kiberiti. Sijui imepangiwa muda gani. Lakini hatimaye haina budi kufikia mwisho kwa kuwa ilikuwa na mwanzo. Naye Mungu pekee Ndiye aliye na Uzima wa Milele. "Yeye ayasikiaye Maneno Yangu, na kumwamini Yeye aliyenipeleka," hana uzima wa *daima*, "yuna Uzima wa Milele." Huo Uzima ulioanza, si kitu chochote kilichoanza *hapa*. Bali njia nzima Kule juu, ni Uzima wa Milele, *Zoe*, Uzima wa Mungu Mwenyewe unashuka na kukaa ndani ya mwanadamu, naye anakuwa ni wa Milele pamoja na Mungu, wala hawezi kufa. Hivyo ndivyo Neno lilivyosema.

229 Wazia tu jambo hilo. Je! kuna Uzima wa Milele wa aina mbili? Usingeweza kujibu hilo, sivyo? Kuna Uzima mmoja wa Milele, na huo ni Uzima wa Mungu. Aina hii nyingine ya uzima, haidhuru ni kitu gani, ina mwisho wake. Na kitu chochote kilichokuwa na mwanzo kina mwisho. Bali kitu chochote kisichokuwa na mwanzo hakina mwisho. Na Mungu alisema atatupa Uzima wa Milele, usio na mwanzo, tulifanywa tu sehemu Yake. Na kwa kweli Uhai ulio ndani yetu, haukuletwa hapa kwa asili ya kibinadamu. Maumbile yalitupa roho fulani, bali hiyo roho ilikufa, nasi tukapata Roho wa Mungu. Utukufu kwa Mungu!

230 Je! Mungu alikuwa ni mwanadamu? Hakika. “Na tumfanye mtu kwa sura yetu.” Mungu alikuwa ni nini? Thiofani, mwili. Na pale mwanadamu alifanywa hivyo na kuwekwa aitawale ile bustani. Bali hapakuwapo na mtu wa kuilima ardhi, aliyekuwa katika hisi. Ndipo akamwumba mtu kutoka katika mavumbi ya nchi, katika uhai wa wanyama, na mtu huyo akailima ardhi. Ndipo huyo mtu akaanguka kwa dhambi. Kweli. Ndipo Mungu, yule thiofani, akashuka na kufanyika mwili na kukaa kwetu, apate kumkomboa mwanadamu.

231 Kwa hiyo si kitu ambacho ungeweza kufanya. Wewe ni mwenye dhambi, kwanza. Umeumbwa katika uovu. Umezaliwa katika dhambi, ukaja ulimwenguni ukisema uongo. Ulizaliwa hapa katika dunia hii kwa tamaa ya kujuana kimwili ya baba yako na mama. Nawe ni wa kuzimu tu kama uwezavyo kuwa, sijali unafanya nini. Huenda kamwe usiseme uongo, kamwe usiibe; ushike kila amri, na chochote kile; nawe utaenda kuzimu, kama mbwayuwayu anavyoenda kwenye sanduku lake. Lakini njia pekee unayoweza kuishi tena, ni kumkubali Roho Mtakatifu, Uzima wa Milele wa Mungu.

232 Ni kitu gani kilichokufanya jinsi ulivyo? Hapo mwanzo, wakati Roho Mtakatifu alipoatamia nchi, hapakuwapo na kitu chochote ila mlipuko wa volkeno. Maskini ua dogo la Pasaka likachipuka. Mungu akasema, “Hilo linaonekana ni la kupendeza sana. Akaendelea tu kuatamia.” Maua yakachipuka. Nyasi zikachipuka. Miti ikaota. Ndege wakaruka kutoka katika mavumbi. Wanyama wakatokea. Mtu akatokea.

233 Sasa, ilifanywaje? Kwa kuatamia kwa Roho Mtakatifu, akivikusanya vitu hivi pamoja, potashi, kalisi; akiumba maua, akiumba mnyama, akikuumba wewe.

234 Na sasa, una uhuru wa kuchagua. Mungu anakuatamia, na kusema, “Unasikia Sauti Yangu? Usifanye mgumu moyo wako, kama katika siku za kukasirisha.” Huyu hapa anashuka, analihubiri Neno.

“Injili waliyohubiriwa haikuninii. . .haikuwa na imani ndani Yake, kwa hiyo haikuwafaa kitu.” Waliisikia, bali hawakuiamini.

235 Mungu alishuka. Aliwaonyesha Nguzo ya Moto. Alionyesha kwa manabii Wake, ishara na maajabu, Yeye alikuwa pamoja naye. Hawakuamini jambo Hilo. Loo, walipenda kuiona miujiza. Walipenda kumsikia nabii. Bali kuhusu kuliamini Hilo, hawakuliamini. Maisha yao yanathibitisha kwamba hawakuamini.

236 “Sasa,” Yeye alisema, “msifuate mfano uo huo wa kutokuamini.” Kwa kuwa katika siku hii ya mwisho, kwa kanisa la Mataifa, Mungu amejitokeza tena; ishara ile ile, ajabu ile ile, Nguzo ya Moto ile ile, imedhihirishwa, imethibitishwa. Na tusiifanye migumu mioyo yetu na kuanguka katika jaribio hilo

huko nyuma, la kutokuamini, kwa kuwa tutaozea duniani na hilo litakuwa ndio mwisho wa yote.

237 Na Roho Mtakatifu anapobisha moyoni mwako, [Ndugu Branham anagonga-gonga mimbarani—Mh.] "Baada ya muda mrefu namna hii, utakapoisikia Sauti Yangu, usiufanye mgumu moyo wako." Akisema, "Ewe mtoto Wangu, hii ndiyo ile Kweli." Usimwangalie mjumbe. Sikiliza Ujumbe. Uamini. "Usiufanye mgumu moyo wako, kama katika siku za kukasirisha."

238 Wakati anaposikia "Sauti Yako," usiufanye mgumu moyo wako. Ndipo unasema, "Naam, Bwana, ninaamini." Ndipo unaingia katika Uzima, Roho Mtakatifu anaingia ndani yako. Roho yako ya kale inakufa, ambayo inakufanya uwe na tamaa mbaya na kuchukia, na kijicho na uadui, na—na chuki na mambo hayo yote, hufa. Nawe unajaa upendo, furaha, amani, ukistarehe. Haidhuru pepo zinavuma jinsi gani, mambo ni shwari.

> Nanga yangu inashikilia ndani ya pazia.
> Katika kila upepo mkali na dhoruba
> Nanga yangu inashikilia ndani ya pazia
>
> Kwa kuwa Kwake Kristo, Mwamba wenye imara, nasimama;
> Ardhi nyingine zote ni mchanga udidimiao.

239 Haya basi. Eddie Perronet, alivyyouandika wimbo huo maarufu. "Ardhi nyingine zote," madhehebu yote, kanuni zote za imani, mafundisho yote, yanatoweka. Kristo!

Unasema, "Vema, ninajua Biblia." Hupati Uzima kwa kuijua Biblia.

"Ninaijua katekismo yangu." Hupati Uzima kwa kuijua katekismo yako.

"Vema, mimi ni Mkristo." Hupati Uzima kwa kukiri Ukristo.

240 Una Uzima kwa kumjua Yeye. Kumjua Yeye, una Uzima. "Ndipo unaingia katika Raha Yake. Unaziacha kazi zako, kama vile Mungu alivyoziacha kazi Zake." Umefanyika Mwana wa Mungu, mshiriki wa Mungu. Na kama huyo—kama huyo Roho Mtakatifu anakubembeleza, nawe unambembeleza na kusema, "Ndiyo, Bwana," ama anakunong'oneza.

241 Anakunong'oneza, "Njoni Kwangu, ninyi nyote msumbukao na mliolemewa na mizigo. Nitawapumzisha."

242 Nawe unasema, "Aa, mimi ni kijana. Nina-. . . Loo, mchungaji wangu haninii . . . Yote ninayopaswa kufanya . . . " Unaona? Kamwe hutampata.

243 Bali unaposema, "Naam, Bwana wangu. Ninaisikia Sauti Yako. Siufanyi mgumu moyo wangu. Sijali, Bwana, ni Neno Lako nami ninakuamini Wewe. Nichukue Yesu. 'hivi nilivyo, bila kujitetea kumoja, bali kwamba Damu Yako ilimwagika kwa ajili yangu. Na hapo nitaahidi, "Nitaamini." Ee Mwana-Kondoo wa

Mungu, ninakuja.'" Weka mikono yako juu ya kichwa Chake kinachokufa, useme, "Bwana, mimi ni mwenye dhambi, Nawe uliniita."

244 "Wote alionipa Baba watakuja Kwangu, Nami nitamfufua katika siku za mwisho."

245 "Naam, Bwana, ninakuja. Siufanyi mgumu moyo wangu, kama walivyofanya katika kule kukasirisha, kwa kweli ninamwamini Yeye."

246 Kwa hiyo Yeye anafanya nini? Anakupa Uzima Wake, *Zoe*, Uzima wa Milele. Na kama Mungu angeweza kutufufua toka katika mavumbi ya ardhi, tulikotoka. . .Je! tulitoka katika mavumbi? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Kila kitu unachoona, kilitoka mavumbini. Na kama Mungu angenifanya kile nilicho leo, bila ya kuwa na chaguo lolote; kwa sababu tu mapenzi Yake yalikuwa ni kuniumba mimi, na kunipa nafasi ya kuikabili Kalvari na kufanya uamuzi wangu; nami nilifanya uamuzi wangu na kumwamini Yeye; ni zaidi sana vipi atanifufua! Kama aliniumba jinsi nilivyo, bila ya chaguo, kisha nikajichagulia na kumwingiza Yeye ndani yangu; wakati alipoweka mikono Yake kwa nafsi Yake, na kuapa kwa nafsi Yake, ya kwamba angenifufua katika siku ya mwisho. Nitakaa na uhakika.

247 Nina Raha, si kwa sababu ninaabudu Jumapili, si kwa sababu ninaabudu kwenye siku ya sabato. Hilo halihusiani nalo. Ninaabudu kwa sababu nimeingia katika amani Yake na Raha Yake: amani, raha, upendo, furaha. Acha dhoruba zipite. Nanga yangu inashikilia.

248 Je! una tukio hilo, usiku wa leo, ewe rafiki yangu unayeketi hapa katika maskani hii yenye joto? Hukuja kunisikiliza mimi. La. Ulikuja kusikia Neno. Sikiliza, ewe rafiki yangu.

249 Sasa kama hujapata Raha hiyo, unaweza kuipata sasa hivi. Haikulazimu kuja hapa madhabahuni. Keti pale pale ulipo. Uwe mwaminifu, na useme, "Kristo, sema tu na moyo wangu. Ninajua kuna joto. Mimi nina—mimi nina jasho jingi tu, ninatokwa na jasho. Niko katika hali mbaya sana. Lakini, Bwana, kwa hakika, huenda nitakuwa nikitoa jasho kwa uchungu, mbaya zaidi kuliko hii, kabla ya asubuhi."

Na huenda daktari akatikisa kichwa chake, aseme, "Ni ugonjwa wa moyo. Ameaga dunia." Vipi basi?

250 Itakuwaje basi? Wakati kile Kitabu kikubwa kitakapofunguliwa, itakuwaje? Mliusikia wimbo huo, *Itakuwaje?* "Wakati wale walioukataa Ujumbe, watakapotakiwa kutoa sababu, itakuwaje basi?" Itakuwaje basi? Wazia jambo hilo sasa, kwa kilindi sana.

251 Tunapoviinamisha vichwa vyetu, wazieni jambo hilo.

Wakati wale wanaoukataa Ujumbe huu usiku wa leo,
Watakapotakiwa kutoa sababu, itakuwaje?
Itakuwaje? Itakuwaje?
Wakati kile Kitabu kikubwa kitakapofunguliwa, itakuwaje basi?
Wakati wale wanaoukataa Ujumbe huu usiku wa leo,
Mtatakiwa kutoa sababu, itakuwaje basi?

252 Baba wa Mbinguni, hili lote limo mikononi Mwako sasa. Hii hapa Sabato ya kweli iliyowekwa mbele za watu. Huyu hapa Malaika wa Mungu, kwa miaka michache iliyopita, ametangaza ulimwenguni kote. Wakosoaji na chochote kile, wamejaribu kuulaani. Lakini, kila wakati, Wewe unajithibitisha kuwa ni Mungu.

253 Ulimwengu wa kisayansi, ulimwengu wa kanisa; je! wao ni vipofu, Bwana? Labda kuna mmoja hapa usiku wa leo angetaka apate kuona, asonge mbele, na asimjaribu Mungu, kama katika zile siku za kukasirisha; si kujaribu kumjaribu, kwa kuwa wazuri Jumapili, ama kuadhimisha siku fulani, ama kwa kuwa na kanuni fulani ya imani, ama kwa kuwa mfuasi wa kanisa fulani. Lakini angependa kuja na kutahiriwa, moyoni, na kumpokea Roho Mtakatifu. Nao wanamtaka Yeye. Kwa imani sasa, wanajaribu kumkubali moyoni mwao. Wanajaribu kupata neema Kwako, Bwana.

254 Loo, huenda walinena kwa lugha. Huenda walipiga makelele. Wangali wana hasira ile ile ya kale. Wangali wana kijicho kile kile cha kale. Wangali wanapiga domo na kupiga soga, na kufanya mambo wasiyopaswa wao kufanya. Hawataki jambo hilo, Bwana. Itakuwaje basi, wakati Kitabu hicho kikubwa kitakapofunguliwa? "Lakini," kasema, "hao hawataingia katika ule Ufalme." "Basi iweni wakamilifu, kama vile Baba yenu wa Mbinguni alivyo mkamilifu." Kitu chochote pungufu hakitaingia. Je! wanatumainia kabisa, usiku wa leo, katika Yeye aliyesulibiwa? Kama sivyo, Bwana, jalia wafanye hiyo "ndiyo" moja ya Milele sasa hivi.

255 Unasema, "Bwana, mimi. . .Si mhemuko, bali ninahisi tu kitu Fulani ndani ya moyo wangu, kwamba kitu Fulani kinaniambia, 'Ninaweza kufanya hivyo sasa hivi, kwa neema Yako.' Na sasa ninakukubali kama Mwokozi wangu binafsi. Nina—ninayakataa mambo yote ya dunia, nami nataka kuingia katika Raha Yako. Nami ninaamini ninafanya hivyo sasa hivi. Ninaamini Roho Mtakatifu ananileta moja kwa moja katika mahali hapo."

256 Wakati kila kichwa kimeinamishwa. Je! kuna mtu yeyote anayejisikia namna hiyo sasa hivi? Inua mkono wako, "Roho Mtakatifu sasa ananiingiza mahali ambapo sitapiga domo

tena." Mungu akubariki. "Sitafanya mambo hayo. Hasira yangu imeondoka. Ninaweza kuishi katika amani na furaha na uvumilivu, tangu sasa hivi. Ninaamini Mungu anazungumza na mimi sasa hivi, ya kwamba ninaweza kufanya hivyo tangu saa hii na kuendelea, kwa neema Yake." Mngeweza tafadhali kuinua mikono yenu? Mungu akubariki. Mungu akubariki ewe msichana. Mtu mwingine? "Sasa naamini."

257 Usimjaribu, kama katika siku ya kukasirisha. Usifikiri ati kwa sababu tunaenda kanisani Jumapili, ama tunaadhimisha sabato. Paulo alisema, "Ninyi mnaoadhimisha siku ama miezi, ama na kadhalika, nawachelea ninyi. Torati ikiwa ni kivuli cha mambo mema yajayo, wala si sura halisi ya kitu hicho, haiwezi kamwe kumfanya mwabuduo awe mkamilifu." Lakini Kristo anakufanya mkamilifu, mkamilifu mbele za Mungu. Anaiondoa dhambi yako, anaondoa hukumu juu yako, anakupa upendo Wake na furaha.

258 Je! ungependa kuingia katika Raha sasa? Mtu mwingine ainue mkono wake, aseme, "Nimefanya hivyo." Mungu akubariki, ewe msichana, hapa kushoto kwangu. Mungu ambariki mwanamume anayeketi kulia kwangu. Kuingia katika Raha Yake, wazia jambo hilo sasa hivi.

259 Omba, "Jinsi tu nilivyo, Bwana, bila ya kuwa na jambo la kujitetea; sifai. Hakuna ninachoweza kukupa Wewe, isipokuwa tu maisha yangu ya kale, yaliyochakaa, yenye dhambi. Je! utanipokea? Utanisafisha? Utaniburudisha? Kwa maana, niliahidi nitaamini. Ee Mwana-Kondoo wa Mungu, ninakuja. Sasa ninakuja, nikiamini sasa ya kwamba nimepita toka mautini kuingia Uzimani. Kwa sababu, papa hapa kitini pangu, nimekukubali Wewe kama Mwokozi wangu na ninasikia amani moyoni mwangu."

260 Watano wameinua mikono yao. Je! mwingine angependa, anayejisikia hivyo, kuinua mkono wako? Kama wewe si Mkristo, mkubali Yesu sasa hivi.

261 Kama unakiri kuwa Mkristo wala hujakuwa wa aina hiyo, wewe ungali ni mwenye dhambi, haidhuru u—haidhuru ni maisha ya jinsi gani umeishi, ama jinsi unavyojaribu kujifanya wewe mwenyewe. Unayofanya hayakubaliwi. Ni yale Yeye aliyofanya. Haki yako mwenyewe haitakubaliwa. Kama ukiacha kuvuta sigara ati kwa sababu tu ulisema, "Vema, afadhali niache kuvuta sigara kwa sababu ninakiri Ukristo." Mungu hakubali hilo. Ukiacha kuwatamani wanawake, ati kwa sababu tu unajifanya mwenyewe kufanya jambo hilo, Mungu hakubali hilo. Hilo ni jambo unalofanya. Hizo ni kazi. Neema ndiyo inayokuokoa. Je! Mungu amekuja kwako na kutoa kitu hicho chote kutoka kwako? Hilo ndilo jambo linalofuata.

262 Unasema, "Nilijiunga na kanisa, na kwa hiyo ilibidi niyaache mambo haya." Mungu hakukubali hilo, hakuna

kitu unachoweza kutoa. Yeye anakubali tu yale Kristo anayotoa. Anakupa Uzima wa Milele, na kukuondolea hayo. Je! utaupokea?

. . . huko kwenye bahari yenye dhoruba, yenye tufani,
Njoo, weka nanga nafsi yako katika kimbilio la Raha,
Na kusema, "Mpenzi wangu ni wangu."
Nimetia nanga nafsi yangu . . .

Vema, unaweza kuinua kichwa chako. Ujumbe umekwisha sasa. Hebu na tuabudu sasa.

Sitaabiri bahari yenye tufani tena;
Dhoruba yaweza kuvuma kwenye bahari yenye tufani kali na kina kirefu,
Katika Yesu mimi ni salama milele.

263 Kila mmoja sasa, katika kuabudu.

Nimetia nanga nafsi yangu katika kimbilio la Raha, (Sabato)
Sitaabiri bahari yenye tufani tena;
Dhoruba yaweza kuvuma kwenye bahari yenye tufani kali na kina kirefu,
Katika Yesu mimi ni salama milele.

Niangazie . . .

Hebu jiachilie tu. Funga macho yako. Unahisi Roho hiyo tamu? Huko ni kuabudu. Ujumbe umekwisha. Huku ni kuabudu.

Jalia Nuru kutoka kwenye mnara wa kuangazia iniangazie,
Ee niangazie, Ee Bwana, niangazie,
Ee jalia Nuru kutoka kwenye mnara wa kuangazia iniangazie.

264 Ni wangapi wanaojisikia vizuri sana? Inua mkono wako. Hiyo roho tamu nyenyekevu, Ndiyo hiyo.

Kuwa kama Yesu, kuwa tu kama Yesu,
Duniani ninatamani kuwa kama Yeye;
Kote katika safari ya maisha kutoka duniani mpaka Utukufuni,
Ninaomba tu kuwa kama . . .

Abuduni tu.

*Kitabu Cha Waebrania*

Jumbe hizi kumi na moja za Ndugu William Marrion Branham zilizohubiriwa hapo awali katika Kiingereza kutoka tarehe 21 Agosti mpaka tarehe 22 Septemba, 1957, katika Maskani ya Branham huko Jeffersonville, Indiana, U.S.A., zimetolewa kwenye kanda za sumaku zilizorekodiwa na kuchapishwa bila kufupishwa katika Kiingereza. Tafsiri hii ya Kiswahili ilichapishwa na kusambazwa na Voice of God Recordings. Ilichapishwa tena katika mwaka wa 2013.

SWAHILI

©2009 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS

P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.

www.branham.org

## Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.


Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:


Voice Of God Recordings
P.O. Box 950, Jeffersonville, Indiana 47131 U.S.A.
www.branham.org